Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 182 | RAM./SHAWWAL 1436 AH | JULAI 2015 | WAFA 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Sema: Ni nani anayewaruzukuni kutoka mbinguni na ardhini? Au ni nani anayemiliki masikio na macho? Na ni nani amtoaye mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima? Na ni nani atengenezaye mambo yote? Bila shaka watasema: Ni Mwenyezi Mungu. Basi sema: Je, hamtaacha kufuata matamanio yenu mabaya? (10:32).

Khalifa Mtukufu Afungua Jalsa Salana ya Ujerumani 2015 na kusema:

Maendeleo ya Jumuiya yadhihirisha Ukweli wa Hadhrat Ahmad a.s.

Na Mwandishi Wetu

Katika Hotuba ya Ijumaa ya leo tutapitia kwa muhtasari, Hotuba ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a. aliyoitoa kwenye sala ya Ijumaa iliyopita huko nchini Ujerumani.

Baada ya tashahud, taaudh na kusoma suratul Faatiha, Khalifa Mtukufu a.t.b.a. alisema:

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Jalsa Salana ya Ujerumani inaanza leo. Jalsa Salana ni sehemu muhimu katika mipango ya Jamaat Ahmadiyya ambayo inafanyika kila pale Jamaat ilipo duniani kote.

Zama zimepita ambapo ilikuwa ni vigumu hata kwa wakazi wa India kuweza kuhudhuria Jalsa Salana ya Qadian.

Sehemu ya Washiriki Jalsa Salana Ujerumani 2015, wakisikiliza Hotuba ya Khalifa Mtukufu.

Kwa kutimiza hilo Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akiwaomba wanajumuiya wajiwekezee kiasi kidogo kidogo ili kiwawezeshe kuhudhuria Jalsa ya Qadian. Leo idadi tu ya magari ya wanajumuiya waishio kwenye nchi za Ulaya yanayofika kwenye Jalsa ni mengi kiasi hiki yanawafanya waandaaji waweke mipango makini kwa ajili ya maegesho. Wazee wa baadhi ya wale waliopo kwenye Jalsa hii, iliwawia shida sana kuweza kuhudhuria kwenye Jalsa, lakini je kuna yeyote leo anayetafakari juu ya neema za Mwenyezi Mungu kwa urahisi na mafanikio aliyowapa na kisha basi hilo likawa njia ya kuwaongezea imani?

Endelea uk. 2

Hatari na Salama zinaowakabili Waislamu

Na Dawati la Kiswahili Morogoro

Mtume Muhammad s.a.w. alibashiri kuwa umati wake utagawanyika makundi 73 na yote yataenda motoni isipokuwa moja tu. Alipoulizwa ni kundi lipi hilo la peponi, akajibu ni lile litakalokuwa juu ya mwenendo wake na wa masahaba zake na litakuwa katika mfumo wa Jamaat. (Tirmidhy Ab waabul iimaan, bab iftiraaqi haadhihil ummati, Bihaarul Anwaar jal. 28 uk. 30 – 31).

Ni nini chanzo cha Waislamu wengi kiasi hicho kupotea na kuwajibika kwenda motoni? Jibu lapatikana ndani ya kauli nyingine ya Mtume Muhammad s.a.w. iliyosimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Amr bin Al Aasw isemayo: Nilimsikia Mtume s.a.w. akisema Mwenyezi Mungu huwa Haichukui elimu kwa mkupuo kutoka kwenye vifua vya watu, bali elimu hutoweka kwa kufariki kwa wenye elimu wenye kutekeleza kwa vitendo hadi kunakuwa hakubakii yeyote mwenye elimu ya uhakika, ndipo watu huwafanya majahili wasiokuwa na matendo mazuri kuwa viongozi, ambao waulizwapo jambo lolote basi hutoa fatwa bila ya kuwa na elimu, wenyewe wanakuwa waliopotea na huwapoteza pia wengine. (bukhari kitabul Ilmi, Bab kaifa yaqbidhul ilma).

Hapa Mtume s.a.w. amebainisha wazi kabisa kuwa wanazuoni wasio na elimu na ucha Mungu ndio watakaokuwa sababu ya upotevu wote huo kutokana na fatwa zao zisizo sahihi. Sehemu nyingine Hadhrat Ali r.a. anasimulia kuwa Mtume s.a.w. alisema: "Itawafikia watu zama ambapo Islamu haitabakia chochote isipokuwa jina lake tu, na Kurani itabakia kuwa maandiko tu, misikiti ya Waislamu itakuwa inajaa waumini lakini ndani hamtakuwa na mwongozo, masheikh wao watakuwa ni waovu kuliko wote waliomo chini ya mbingu, fitna zitakuwa zinachimbukia kwao na kuwarejea." (Mishkaat Kitabul Ilmi. baabul iimaan cha Imam Baihaqiy. Na Al Furuu min Jaamiil Kaafii, jal. 3 uk. 144).

Hadhrat Hudhaifa bin Yaman pia anasimulia kwa kusema: 'Watu walikuwa wakimuuliza Mtume s.a.w. mambo ya kheri na mimi nilikuwa nikimuuliza mambo ya shari nikihofia yasinikumbe, hivyo nikasema: Ewe Mtume wa Allah! Sisi tulikuwa katika zama za kijahili na za shari, basi Allah Akatuletea heri hii ya Uislamu. Je itatokea shari yoyote baada ya heri hii? Akasema ndio. Nikauliza tena je baada ya shari hiyo kutakuwa tena na heri? Akasema ndio ila itakuwa na madoa. Nikamuuliza ni madoa yepi hayo? Akasema watakuwepo watu watakaowaongoza watu kinyume na mwongozo wangu. Utapendezwa na baadhi ya matendo yao na utachukizwa na baadhi ya matendo yao mengine. Nikauliza tena je kutakuwa na shari baada ya heri hiyo? Akajibu ndio, kutakuwa na watu watakaokuwa wakiwaita watu kwenye milango ya Jahannam na yeyote atakayewaitikia watamtumbukiza ndani ya moto wa Jahannam. Nikamwambia; Ewe Mtume wa Allah, tufafanulie watu hao walivyo. Akasema: Watatokana na watu wetu na wataongea lugha yetu. Nikamuuliza waniamuru nini kama mambo hayo yatatokea katika uhai wangu? Akajibu; ushikamane na jumuiya ya Waislamu na Imamu wake. Nikauliza: Kama hakutakuwepo na Jumuiya ya Waislamu wala Imamu? Akajibu basi uyaepuke madhehebu yote hata kama ulazimike kula mizizi ya miti hadi mauti yakufike ukiwa katika hali hiyo." (Bukhari Kitabul Fitan, Bab Kaifal Amru idhaa lam takun Jamaatun).

Hapa Mtume s.a.w. alibainisha wazi kwamba upotevu utabainika kwa Waislamu kuwa na madhehebu mengi yaliyohitilafiana na akanasihi kwamba anayetaka kuongoka

Endelea uk. 3

Mapenzi ya Mungu
Maoni ya Mhariri

HOMA YA UCHAGUZI

Hakuna kielelezo bora cha heshima ya binadamu kama uhuru aliopewa wa kuchaguwa. Ni dunia ya kuchagua. Na mtu hatakiwi kuingiliwa katika uhuru huo wa kuchagua. Na katika maisha kila mtu hufikia njia panda. Na kwa sababu mtu mmoja hawezi kutembea njia mbili humbidi afanye uteuzi wa njia atakayopitia.

Uhuru huo tumepewa na Allah. Binadamu hakulazimishwa bali amepewa uhuru wa kusikiliza hoja na kuchagua. Hiyo ndiyo maana ya 'Shaakiran ama kaafura' (Shukuru au kufuru). Na jambo linalotawala maisha yetu yote ni jambo hilo la kuchagua. Lakini linataka uangalifu sana. Ukweli ni kwamba rasilimali ni chache lakini mahitaji yetu ni mengi. Hivyo tunalazimika kufanya uchaguzi. Kwa mathalani kazi zipo nyingi duniani na hivyo mtu analazimika kuchagua kazi anayoipenda na kuimudu.

Katika mnasaba huo taifa letu limo katika hali ambayo tunaweza kuipa jina 'Homa ya Uchaguzi'. Kila kinachofanywa sasa hivi nchini mwetu kina ujumbe mmoja tu nao ni 'Uchaguzi'. Ofisi zipo tupu sababu uchaguzi. Hotuba zinatolewa shauri ya uchaguzi. Nguo zinavaliwa lakini si hivi hivi nazo zina ujumbe ni sehemu nyingine ya uchaguzi. Na hayo yote yanaongeza homa ya uchaguzi.

Ni lazima ieleweke kwamba hali hiyo si mbaya hata kidogo. Ni gharama ambayo tunatakiwa kulipa ili kuwapata viongozi watakaotutangulia na kuonesha njia. Bila shaka katika harakati hizo ni vizuri na busara kukumbuka la juu kuliko yote na lenye thamani ni mama yetu Tanzania. Wa kumlinda mama huyu na kudumisha sifa yake ni sisi Watanzania. Katika kufanya hivyo tofauti zetu za dini, kabila, rangi, itikadi kamwe visitumike kwani vitatucheleweshe. Na hatimaye kuigawa nyumba hii katika sehemu mbili. Na nyumba iliyogawika katika sehemu mbili katu haiwezi kusimama. Wakati huu kuliko wakati wowote ule tuyape haki yake masikio, tujaribu kusikiliza, tujitahidi kuhudhuria mikutano ya vyama ili tuelewe na kupima sera na uwezo wa mtu binafsi na chama anachowakilisha.

Uwezo wa mtu kusema katu usituyumbishe, la msingi ni kuelewa vitendo vya msemaji kwani wasemavyo waswahili; "Ada ya mja hunena, Muungwana ni vitendo'. Kiongozi aliyetuahidi mambo ya kujaza kikapu na leo hatuoni hata moja hivyo apewe fursa ya kupumzika kwani mti hujulikana kwa matunda yake. Tumekuwa na wabunge tumeona mbwembwe zao, tumesikia mawazo yao, tumewasikia wakichangana maneno ya Kiswahili na Kiingereza wakati wakijua fika wapo wapiga kura wao ambao hawajui hata neno moja la Kiingereza. Tunahitaji viongozi wanaojua walikotoka na watu waliowaacha nyuma. Kusahau tuliko toka ndiko kunasababisha mtu kuweka maneno ya Kiingereza ambayo hayafikishi ujumbe kwa wapiga kura wengi. Tunahitaji viongozi mahiri wanaoenzi na kuthamini Kiswahili. Kwani ni kwa kupitia lugha hiyo tu ndipo tunaweza kuwasiliana na kuelewana. Dua zetu ni kwamba tupate viongozi wanaosikiliza wanyonge na kuwatumikia. Tunataka kupata viongozi watakaokuwa na ujasiri wa kunukuu waandishi wetu akina Shaabani Robert, Mathias Mnyampara n.k hakuna faraja kubwa kama kuona mtu anaienzi na kuthamini lugha yetu ya Kiswahili.

Tunataka viongozi ambao wanaelewa kwamba dunia hii sio mwisho, bali nimwanzo wa mwisho. Na kwamba vitendo vyetu vyote hapa duniani bila shaka kuna maswali ambayo tutayajibu. Na kiongozi anakuwa na dhamana kubwa zaidi kwani ana wengi ambao anawachunga. Hivyo ataulizwa alivyowatendea wale aliopewa dhamana ya kuwachunga. Tunataka viongozi wanaokusanya pamoja na sio wale wanaotawanya. Tunahitaji viongozi ambao maumivu yetu ni maumivu yao. Tunawataka viongozi ambao ni watumishi na sio mabwana. Allah Atubariki tupate viongozi wa sampuli hii.

Tunataka viongozi wenye uwezo wa kutizama katika mbegu ya wakati na kutueleza mbegu itakayoota na ile ambayo haiwezi kuota. Tunataka viongozi ambao hawatouliza Tanzania itawapa nini, bali wao wataipa nini Tanzania.

Jalsa salana Ujerumani 2015

Kutoka uk. 1

Je, tunajitahidi kuwa na imani na maungano na Mwenyezi Mungu ambayo wazee wetu walikuwa nayo? Baadhi ya wazee wetu waliokuwepo wakati wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na ambao walimuamini walitamani sana waweze kumtembelea lakini walishindwa kutokana na kutokuwa na uwezo kifedha. Wakati ambapo leo watu wanatoka nchi za nje kwa gharama zao kuhudhuria Jalsa ambayo mtumishi na Khalifa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. yupo. Si hivyo tu bali kuna wanaotafuta ukweli ambao hawajajiunga na Ahmadiyyat nao pia wamesafiri kutoka nchi mbalimbali kuhudhuria katika Jalsa.

Wakati ni jambo linalochangamsha nyoyo kwamba mambo yamebadilika kuwa mazuri na ujumbe wa Mwenyezi Mungu unaenea zaidi na zaidi duniani, familia za wazee wa mwanzo ndani ya Jamaat zitafakari iwapo zinacho kiwango kile cha maungano na Mwenyezi Mungu, imani na kutii amri za Mwenyezi Mungu ambacho wazee wao walikuwa nacho. Ni jambo la kutia hofu iwapo kuna kuanguka katika jambo hili. Tunaweza kuwa na mafanikio kwenye mambo ya kidunia lakini kwenye maswala ya kiroho tukawa ni debe tupu. Katika baadhi ya nyakati mtu huweza kuzama kwenye mambo ya kidunia na kuishia kwenye mkamato wa shetani kiasi hiki kwamba kushiriki kwake kwenye Jalsa kunakuwa ni sherehe ya kidunia tu. Juhudi zifanyike kubaini mapungufu yetu wakati wa Jalsa na kisha tukusudie kujirekebisha zaidi. Tumuombe sana Mwenyezi Mungu kwamba sisi na vizazi vyetu tusiwe wenye kushikwa na ghadhabu za Mwenyezi Mungu.

Jamaat inaendelea kupanuka kwani Mwenyezi Mungu anazifungulia nyoyo na kuwawezesha watu kujiunga nayo. Mwenyezi Mungu awajaalie wale wote wanaojiunga na Jamaat kwa lengo la kusafisha imani zao, basi watimize pia matakwa ya kushiriki Jalsa.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametuambia kwamba lengo la Jalsa Salana ni kukuza maungano na Mwenyezi Mungu, mtu kuishi maisha yake yote kwa kutimiza amri za Mwenyezi Mungu, kutimiza haki za ndugu zake, na kutangaza ujumbe wa Mwenyezi Mungu duniani. Matakwa yote haya yanahitaji kujitoa mhanga. Jalsa Salana sio tamasha la kidunia na wala sio njia ya kupata malengo ya kidunia.

Watu wanaohudhuria Jalsa wajibidiishe kumdhukuru sana Mwenyezi Mungu muda wote. Kumkumbuka Mwenyezi Mungu kufanywapo na mtu binafsi kunakuwa na manufaa kwake yeye na kwa jamaat kwa ujumla. Faida nyingine ya kumdhukuru Mwenyezi Mungu ni hii kwamba watu wengine nao hukumbushwa kumkumbuka Allah badala ya kujiingiza kwenye maongezi yasiyo na maana. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu matendo yafanywayo wakati wa Jalsa huacha athari kubwa nyoyoni kwa muda, na kama mtu ataendelea kuyazingatia athari yake inaweza kudumu kwa muda mrefu zaidi. Siku za Jalsa zitumike kama vile ambavyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametuongoza na kutarajia kutoka kwetu.

Kukuza maungano na Mwenyezi Mungu, na kuzijaza nyoyo na huruma kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu. Kutokuelewana kokote baina ya watu kurekebishwe wakati wa Jalsa. Tutaweza tu kuupeleka ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wengine katika maana ya kweli ya kufikisha ujumbe pale tu tutakapokuwa na maungano ya kweli Naye. Hata hivyo, njia zote hizi zinahitaji uimara mkubwa.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema dunia hii ni ya mpito na siku moja itatoweka. Ni ya muda tu sawa na mipango ya Mwenyezi Mungu. Hivyo basi tujitahidi kukimbilia kwenye uelewa sahihi na maungano na Mwenyezi Mungu. Iwapo tutatembea hata kwa mwendo mdogo, Yeye atatupokea kwa mwendo wa kasi, ingawaje, hatua ya kwanza lazima ifanywe nasi wenyewe.

Baadhi ya watu hulalamika kwamba wamejaribu njia mbalimbali kuanzia kusali, kufunga na namna zingine za ibada na kukua kiroho lakini hawajafikia popote. Hii imetokana na asili yao ya kutilia shaka. Haiwezekani kwa Mwenyezi Mungu kukiwacha kitu chochote kipotee bure ambacho kimefanywa kwa ikhlasi kwa ajili yake na kwamba asikilipe kitu hicho hapa hapa duniani. Iwapo lengo la matendo yetu ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu basi kwa hakika tutapata radhi Zake. Tujitahidi kujitoa kwenye giza la kidunia na kukusudia kwa moyo wote kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Ni fadhili za Mwenyezi Mungu juu yetu kwamba anawatuma wale Anaowachagua, ambao ni watu wateule juu ya ardhi na pia sisi tunayo bahati kubwa ya kumkubali yule aliyetumwa na Mwenyezi Mungu zama hizi. Amekuja na ametufunza juu ya haki za Mwenyezi Mungu na haki za viumbe wa Mwenyezi Mungu na ametukumbusha juu ya kujiepusha na maovu yote iwe ya mtu binafsi au ya jamii. Iwapo baada ya kuchukua Baiat hatuyazingatii mambo haya tutakuwa hatujatimiza wajibu wetu. Mitume wa Mwenyezi Mungu wanakuja ardhini kuleta mapinduzi. Mwenyezi Mungu alimuonesha Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwenye njozi kwamba anaumba mbingu mpya na ardhi mpya na kisha akatakiwa amuumbe mtu mpya. Hii bila shaka ilikuwa ni oneshao la mapinduzi atakayoleta.

Onesha lililokamilika la kuumba mbingu mpya na ardhi mpya lilioneshwa na Mtume Mtukufu s.a.w.. Alikuja miongoni mwa watu ambao hawakuwa na hata alama ya dhana ya Mungu mmoja lakini kutokana na baraka za mapinduzi aliyoleta watu hawa wakabadilika kiasi hiki kwamba umoja wa Mungu ukawa ni lishe bora kwao kuliko chakula cha kidunia. Wanawake wa zama zake pia wakasonga mbele katika kumcha Mungu. Mama mmoja miongoni mwa masahaba zake alikuwa amefunga kamba kutoka darini ili imsaidie asilale wakati wa Kumuabudu Mungu. Masahaba walijitolea mali zao kuwapatia wengine wajiendeleze kimaisha ili wao wapate muda zaidi wa kujitolea katika njia ya Mungu. Pia walionesha viwango vya hali ya juu vya uaminifu. Haya yote yalitokea kwa sababu ya mabadiliko ya kimapinduzi yaliyoletwa na Mtume mtukufu s.a.w.. Kwa hakika aliwaheshimu kinamama na kuwapatia haki zao katika jamii ambayo hawakuwa na hadhi yoyote.

Hazrat Musleh Mauud r.a. aliilinganisha jamii ya leo na ile ya zama zile. Akasema katika siku za nyuma mwanamume alimdhalilisha mwanamke na kumfanyia vitendo vya mateso na kumuhesabu asiye na haki yoyote. Mwanamume aliendelea kumdhalilisha mwanamke hata huko Ulaya

Endelea uk. 4

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Hatari na Salama zinaowakabili Waislamu

Kutoka uk. 1

atalazimika kujiepusha na madhehebu yote hayo na alitafute kundi litakalokuwa na nidhamu ya kuongozwa na Imamu mmoja mwenye lakabu ya Khalifa.

Aina ya Imamu huyo imefafanuliwa zaidi na Mtume s.a.w. ndani ya kitabu cha Maswnad Ahmad bin Hanbal, jal. 5 uk. 403, chapa ya Kiarabu iliyochapishwa na Dar ul Fikr ya huko Beirut, pale Mtume s.a.w. aliposema: "Kama, katika zama hizo za wale wenye kuwaita watu kwenye upotevu na kwenye madhehebu mbali mbali, utamuona Khalifa yeyote wa Mwenyezi Mungu, basi ushikamane naye hata kama upigwe na uporwe mali yako."

Kauli hii ya Mtume s.a.w. inaeleweka zaidi kwa kuisoma kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: Allah Amewaahidi walioamini na kufanya vitendo vizuri kati yenu, kuwa Atawafanya Makhalifa katika ardhi, kama Alivyowafanya Makhalifa wale wa kabla yao, na Atawaimarishia dini yao Aliyowaridhia (Islamu), na Atawabadilishia hofu yao kuwa amani, wataniabudu na hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo (atakayekataa kushikamana na nidhamu hiyo ya ukhalifa), basi hao ndio wavunjao amri. (24:56)

Hii ni nasaha nzito sana kwetu sisi Wanadamu, kwamba tujiepushe kabisa kushikamana na madhehebu mbali mbali, bali tuitafute jumuiya ya Kiislamu yenye kuongozwa na Imamu mmoja mwenye daraja la Khalifa na kushikamana nayo kwa nguvu zote. Ukhalifa huo hautotofautiana na ukhalifa ule uliopatikana hapo zamani, ambamo hata Makhalifa wenye madaraja ya unabii na utume walipatikana (Swad : 27, Baqara : 31) pamwe na Makhalifa watawa na wanazuoni waliokuwa sio manabii (5:45).

Mwenyezi Mungu hapa Amefafanua kwa ufasaha kabisa kuwa dini ya Islamu itaimarika chini ya uongozi huo wa Ukhalifa, Waislamu wataondokewa na hofu yao na kuzingirwa na amani kama wataukubali uongozi huo wa ukhalifa, na ibada ya kweli isiyo na ushirikina, itakayokubalika mbinguni ni ile itakayofanywa chini ya uongozi huo wa ukhalifa. Mwishoni Amemalizia bila ya kuuma maneno kuwa wote wale watakaokataa kuwa ndani ya uongozi huo ulio chini ya nidhamu ya ukhalifa, watahesabiwa kuwa ni waasi wavunjao amri.

Mtume s.a.w. alitupatia taarifa zisizo na shaka yoyote kuwa katika siku zetu hizi za mwisho, Mwenyezi Mungu Atamleta Isa bin Mariamu atakayekuwa pia ni Imamu Mahdi, atakayetokana na Waislamu wenyewe. Hadhrat Abu Huraira anasimulia kuwa Mtume s.a.w. alisema: "Mtakuwaje atakapokushukieni Isa mwana wa Mariamu naye atakuwa Imamu wenu atakayetokana nanyi." Na ndani ya Muslim imesemwa kuwa "Isa huyo huyo atawaongozeni akiwa Imamu wenu atakayetokana nanyi" akitumia Kurani na Sunna za Mtume s.a.w..

Pia alisema: "Mahdi ndiye huyo huyo Isa." (Ibnu Maajah, Kitabul Fitan, babu shiddatiz zamaan).

Sehemu nyingine alisema "Huenda atakayeishi kati yenu akakutana na Isa mwana wa Mariamu akiwa ndiye Imam Mahdi na hakimu mwadilifu." (Masnad Ahmad bin Hanbal, jal.2, uk. 411 chapa ya Dar ul Fikr, Beirut).

Mtume Muhammad s.a.w. alisema pia kuwa huyo nabii Isa a.s. atakayekuja atakuwa ni Khalifa wake atakayetokana na umati wake Mtume Muhammad s.a.w. pale aliposema: "Sikilizeni! Hakika yeye atakuwa ni Khalifa wangu ndani ya umati wangu." (Al muujamus swaghiir, juzu ya 1, uk. 257 kilichoandikwa na Allama Twabrani na kuchapishwa na Dar ul fikr, Beirut).

Halikadhalika alisema kuwa utakuja ukhalifa wa njia ya wazi ya unabii (Masnad Ahmad bin Hanbal, jal. 4, uk. 273 kilichochapishwa na Dar ul fikri Beirut na pia yapatikana Hadithi hii ndani ya kitabu cha Mishkaat, bab ul indhaari wat tahdhiir).

Hii yatuthibitishia kuwa makhalifa kama wale waliopatikana zamani, ambapo baadhi yao walikuwa na madaraja ya unabii, watapatikana pia miongoni mwa Waislamu, sambamba na ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyomo ndani ya Sura Annur : 56.

Hayo yanaweza kutupa mwanga kwamba kwa nini Mwenyezi Mungu Ametulazimisha tuombe zaidi ya mara hamsini kila siku dua ya kumuomba Atuongoze kwenye njia iliyonyooka, ya wale Aliowaneemesha na Atuepushe kuelekea kwenye njia ya wale waliokasirikiwa na kupotea.

Mojawapo ya njia zilizonyooka ipatikanayo ndani ya Kurani Tukufu ni ile iliyotajwa ndani ya Sura 2:214-215 ambapo Mwenyezi Mungu Anafahamisha kuwa, watu wa umati mmoja wanapoyaasi mafundisho yao na hatimae kufarakana na kuwa makundi kwa makundi yenye kuhitilafiana, basi hapo, sawa na desturi yake isiyobadilika (35:44), Huteua manabii miongoni mwao na Kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka wale wanaowakubali mitume hao wanaokuja kuwaongoza baada ya kutokea hitilafu ndani ya umati.

Anasema Watu walikuwa umati mmoja, basi Allah Akawainua Manabii wenye kuleta habari njema na kuonya, na Akateremsha pamoja nao Kitabu kwa haki, ili Ahukumu baina ya watu katika yale waliyohitilafiana, na hawakuhitilafiana kwacho isipokuwa wale waliokipewa baada ya kuwafikia ishara zilizo bayana kutokana na uasi uliokuwa kati yao. Basi Allah Akawaongoza wale walioamini katika yale waliyohitilafiana katika haki kwa idhini Yake, na Allah Humuongoza Amtakaye katika njia iliyonyooka. (2 : 214). Hapa njia iliyonyooka ni ya wale wanaowakubali na kuwaamini manabii wanaotumwa na Mungu wakitokea ndani ya umati wa watu walioyaacha mafundisho yao sahihi na kufarakana katika makundi tofauti, hawa ndio huwa juu ya mwongozo ulio sahihi.

Aya inayofuatia yatutahadharisha tusidhani kuwa hali hiyo iliyotokea ni kwa ajili tu ya watu wa nyimati zilizopita, bali hata sisi zitatufikia zama kama hizo za kufarakana na kuwa makundi makundi kutokana na kuyaasi mafundisho yetu ya kiislamu, kama vile alivyobashiri Mtume s.a.w. katika Hadithi hiyo hapo mwanzoni. Na leo kila mmoja ni shahidi kuwa waislamu tumefarakana na kuwa makundi makundi yenye kuhasimiana na hata kuuana hovyo kabisa, kinyume kabisa na mafundisho yetu yenye kuhimiza sana upendo na amani.

Hali hii, sawa na sunna ya Mwenyezi Mungu isiyobadilika, kwamba idadi kubwa ya watu inapopotea, Mungu Huleta waonyaji kati yao (37:72), kuwa hatutaweza kuingia peponi mpaka tufikiwe na mfano kama ule uliowakumba wale wa kabla yetu, ambapo wale waliowaamini manabii waliowadhihirikia baada ya kutokea uasi na hitilafu miongoni mwao, mtume yule na wale waliomwamini wakadhikishwa mno, kama aya hiyo isemavyo:

Je mnadhani mtaingia peponi kabla haujawafikia mfano wa wale waliopita kabla yenu, ziliwashika shida na madhara mpaka mtume na wale walioamini pamoja naye wakasema ni lini msaada wa Allah utakuja? Basi sikilizeni msaada wa Allah upo karibu (2 : 215).

Wanaoamini pamoja naye mradi wake ni kwamba, katika makundi yote hayo ya umati husika, watakapokuwa wamefikia kwenye kilele cha upotevu na mfarakano, kundi litakalokuwa na imani yenye kukubalika mbinguni, inayoafikiana na mwongozo uliomo ndani ya Kitabu cha umati huo, litakuwa ni lile la Mtume huyo na wafuasi wake, ambao moja ya alama yao kuu ni kuteswa kwao mno na kusumbuliwa kupita kiasi, wakipewa kila aina ya madhara pamwe na kutengwa na makundi yote hayo, lakini juu ya yote hayo litaonyesha subira ya hali ya juu wakiwa na matumaini makubwa ya msaada wa Allah.

Hivyo kundi lile la peponi lililobashiriwa na Mtume s.a.w., ni lile litakalokuwa ndani ya nidhamu ya ukhalifa ulioibukia toka kwenye unabii.

Njia hiyo ilyonyooka tuliofundishwa tuombe kungozwa juu yake, ni njia ile ile waliyoipita wale walioneemeshwa na Mwenyezi Mungu, ambapo sura ya An Nisaa aya ya 70 imebainisha kuwa wenye kumtii Allah na Mtume Muhammad s.a.w. ipasavyo, watathibitika kuwa wako juu ya njia hiyo, kwa kupatikana ndani mwao, neema hizo zilizoorodheshwa za unabii, uswiddiq, ushaahid na uswaalih. Aya hiyo yasema hivi: "Na wenye kumtii Allah na Mtume s.a.w., basi hao ni miongoni mwa wale Aliowaneemesha Allah, Manabii, maswiddiq, Mashaahid na Maswaalih, na hao ndio marafiki wema."

Kinyume na hao sio marafiki wema hata kidogo, bali tumefundishwa tuombe katika kila rakaa, kila siku, dua ya kuepushwa kuifuata njia yao, ambayo Mwenyezi Mungu Ameitaja kuwa ni njia ya wale waliokasirikiwa na kupotea.

Miongoni mwa njia hizo za waliopotea na kukasirikiwa na Mwenyezi Mungu zimezobainishwa na Mungu mwenyewe ndani ya Kurani Tukufu, ni njia ile waliyoipita watu wa Yusuf imeyobainishwa katika sura ya (40 : 35 – 36) ambao walidai kuwa Mungu Hatotuma tena Mtume mwingine baada ya Yusuf, kauli ambayo Mungu Ameisema hutamkwa tu na watu Ameowathibitisha kuwa ni wapotevu na ni kauli inayomuudhi sana Mwenyezi Mungu na pia yenye kuwaudhi mno wale waaminio wa kweli.

Anasema Mwenyezi Mungu: "Bila shaka hapo kabla aliwafikieni Yusufu kwa ishara zilizo wazi, lakini mkadumu kuwa katika shaka juu ya yale aliyokujieni nayo, mpaka alipofariki, mkasema; Allah Hataleta tena Mtume baada yake. Kama hivyo Allah Huthibitisha upotevu wa yule aliyeruka mipaka, ambao hujadiliana katika aya za Allah bila ya dalili yoyote iliyowafikia. Ni chukizo kubwa mbele ya Allah na mbele ya wale walioamini. Hivi ndivyo Allah Apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa mjeuri, ajitukuzaye." (Sura Al Mu'umin : 35 – 36).

Hivyo itikadi kama ya watu wa Yusuf ya kudai kuwa Mungu Hataleta Mtume yeyote baadae, sawa na aya hizo hapo juu, ni itikadi ambayo Mungu Ameisema na kuithibitisha kuwa ni ya upotevu na ni yenye kumuudhi mno. Itikadi hiyo, sawa na aya hii, ni ya watu majeuri wenye kujitukuza na Mungu Amepiga muhuri juu ya mioyo ya watu wa aina hiyo. Ndani ya Sura Baqara Mungu Anasema kuwa Yeye Hupiga muhuri juu ya makafiri waliobobea ambao hata wakionywa au wasionywe wanakuwa si wenye kuamini. Itikadi hii ipo juu ya njia tumeyofundishwa tuombe zaidi ya mara hamsini kila siku kuiepuka kwa kuomba; Ghairil maghdhuubi 'alaihim wala dhwaalliin yaani utuepushe kuelekea kwenye njia ya wale waliokasirikiwa na kupotea. (Sura Alhamdu : 7).

Pia Mungu Ametuahidi ndani ya Kurani Tukufu kuwa Atawafanya kuwa Makhalifa wale waaminio wa kweli wenye vitendo vizuri vinavyokubalika mbinguni na makhalifa hao watakuwa kama wale makhalifa wa kabla yao, ambao baadhi yao walikuwa ni Makhalifa waliokuwa na madaraja ya unabii, kama vile Adam na Daud a.s. (2:31) na baadhi yao walikuwa ni Makhalifa waliokuwa na madaraja tu ya uanazuoni na utawa, bila ya kuwa manabii, (5:45).

Kwa hiyo kama kuna kundi lolote miongoni mwa Waislamu lililoanzishwa na mtu aliyedai kuwa ni nabii, na kama limefanikiwa kuwa na nidhamu ya ukhalifa kama ule uliokuwepo hapo kabla jinsi umevyobainishwa ndani ya Kurani Tukufu, na kama kundi hilo liko peke yake lenye nidhamu hiyo ya ukhalifa na liko peke yake na itikadi iliyo kinyume na itikadi kama ya watu wa Yusuf, kwamba neema ya unabii na utume inaendelea baada ya Mtume s.a.w., na kama makundi yote ya Kiislamu yameungana kulipinga kundi hilo lililofanikiwa kuwa na neema hizo za kiroho zilizobashiriwa ndani ya vitabu hivi vitakatifu, basi itapaswa kuitafakari na kuizingatia Hadithi ile ya Mtume s.a.w. iliyosema kuwa umati wake utagawanyika katika makundi 73 na yote yatakuwa ya motoni isipokuwa moja tu litakalokuwa na mwenendo kama wake na wa masahaba zake, ambao walidumu ndani ya nidhamu ya ukhalifa kwa kuwa na Khalifa aliyewaongoza katika masuala yote ya kiroho.

Ndugu wapendwa! Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ni kundi pekee miongoni mwa makundi yote ndani ya Islamu lenye kuongozwa na nidhamu ya Ukhalifa kama ule uliokuwepo hapo kabla (5:45). Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. (1835 – 1908) aliutangazia ulimwengu kwamba Mwenyezi Mungu Amemtuma kuja kuuongoza ulimwengu kwenye mwongozo sahihi kama ulivyofundishwa na Manabii wote wa Mwenyezi Mungu na kukamilikia kwa Mtume Muhammad s.a.w. Alisema kwamba yeye ndiye yule yule Imam Mahdi na Masihi Isa ambaye Mtume s.a.w. alitoa bishara za kuja kwake katika zama zetu hizi za mwisho. Mwaka 1894 na 1895 Mwenyezi Mungu Alithibitisha ukweli wa madai yake haya kwa jua na mwezi kupatwa ndani ya tarehe maalum za mwezi wa Ramadhani kama

Endelea uk. 4

Khalifa Mtukufu Afungua Jalsa Salana ya Ujerumani 2015

Kutoka uk. 2

Sehemu ya Washiriki Jalsa Salana Ujerumani 2015, wakisikiliza kwa makini vipindi vilivyokuwa vinaendelea wakati wa Jalsa.

ambako uhuru leo unashikiwa bango. Tofauti ya zama zilizopita na zama za leo ni hii tu kwamba pamoja na kuwadhalilisha na kuwatesa wanawake, leo wanaume husema kwamba si haki kumtesa mwanamke. Hivyo kimsingi matendo ya wanaume yamebaki yaleyale ingawaje msemo umebadilika.

Mtume mtukufu s.a.w. alileta mapinduzi yaliyokamilika katika nyanja zote za maisha. kwa hakika ulikuwa ni muujiza mkubwa ulioletwa naye wakati watu wasiokuwa wa Mungu wakabadilika kabisa na kuwa watu wa Mungu. Hii ilikuwa ni ardhi mpya na mbingu mpya iliyoumbika kwa kuja kwake. Katika zama hizi Mwenyezi Mungu amemuagiza Mtumishi mwaminifu wa Mtume mtukufu s.a.w. asonge mbele kuumba dunia mpya na mbingu mpya. Je watu leo ni sawa na wale waliomzunguka Mtume mtukufu s.a.w..? Bila shaka siyo hivyo. Kwa hakika ujinga wa kabla ya Uislamu unaonekana kuzuka upya na hii ndio sababu Mwenyezi Mungu akamtuma Masihi Aliyeahidiwa a.s. sawa na ahadi Yake. Kulikuwa na zama ambapo Uislamu ulifuatwa kikamilifu kwa utukufu wake wote lakini Waislamu wa leo wanayasujudia hata makaburi.

Bila shaka wanaendelea kutamka kwamba Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah .. lakini kauli hiyo haileti mabadiliko yoyote mema ndani mwao kwa sababu hawaelewi maana yake. Ni waislamu lakini kwa jina tu. Kuna wengi miongoni mwao ambao hukiri kuwa watumishi wa Mungu mara tano kwa siku, lakini mwenendo wao ni wa kishirikina.

Wengi wa wasomi wakubwa wa huko Pakistan hutembelea makaburi ya watawa na kufanya mambo ya kishirikina. Makundi ya wenye misimamo mikali na taasisi zingine zimeanzishwa kwa jina la Islam, ambapo inaonekana kutambua neno moja tu "Jihad" lakini na hilo pia wanalielewa kimakosa ambapo huwafanya watu wawe mbali zaidi na dini. Ilikuwa ni wakati hasa unaohitaji Masihi kudhihiri ili kutengeneza dunia mpya na mbingu mpya na kwa hakika amelidhihirisha hilo.

Mtu mmoja alimuuliza mtu ambaye zamani alikuwa ni mwizi mkubwa kuwa kuna ishara gani ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Mtu yule akajibu kwamba: "Mimi mwenyewe ni ishara ya ukweli wake kwani tangu nilipomkubala Masihi Aliyeahidiwa a.s. nimebadilika kabisa na nimewacha wizi wote". Kwa hakika Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametengeneza ardhi mpya na mbingu mpya katika zama hizi na ameyabadilisha maisha ya mamia ya maelfu ya watu wakidhihirisha ni vipi ardhi mpya na mbingu mpya yaweza kutengenezwa. Ingawaje njozi yake hiyo pia inawakumbusha wanajumuiya wa Jamaat yake kuonyesha ni juhudi gani na makusudio gani wayashike juu ya hili baada ya kufanya kwao Baiat.

Je tunajitahidi kufikia viwango vya ardhi mpya na mbingu mpya ambavyo masahaba walivifikia kwa kuyafuata mafundisho ya kweli ya Islam. Je roho zetu zimepata mabadiliko chanya ambayo yanawafanya watu wakiri kwamba watu hawa wameumbika kwenye ardhi mpya na mbingu mpya? Iwapo tunataka dunia ione dhihirisho la ardhi mpya na mbingu mpya iliyotengenezwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ushahidi mkubwa unatakiwa uwe ni mfano wetu sisi wenyewe. Kumkubali kwetu Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakutakiwi kuishie tu kwenye masuala ya kiimani bali kwa hakika mabadiliko chanya kwenye matendo yetu yanatakiwa yawe bayana.

Hazrat Musleh Maud r.a. aliwahi kusema kwamba ishara za Masihi Aliyeahidiwa a.s. ziko za aina mbili. Kutimia kwa aina moja kumo mikononi mwa Mwenyezi Mungu moja kwa moja lakini kutumia kwa aina ya pili kunategemea pia juhudi tunayoiwekeza na kunatimia kupitia sisi. Kwa hakika tunatakiwa tufanye jitihada kubwa katika kutimia kwake.

Kuna mambo mengi ambayo ni Manabii wa Mungu tu ndio wanaoweza kuyaelewa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alifafanua mambo mengi ambayo kwa kipindi cha miaka 1400 yalipokuwepo hakuna mwanaulamaa aliyewahi kueleza maana ya kweli ya mambo hayo. Kwa mfano suala la kwamba dini zote za dunia kiasili ni za kweli hata kama mafundisho yake yalichafuliwa baadaye. Buddha, Zoroaster na Krishna wote walikuwa ni wakweli. Watu wanaofata mafundisho ya kweli ya viongozi wao bila shaka wanakuwa na hali bora kuliko wengine. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akafafanua kwamba mafundisho ya Manabii wote wa kabla yalikuwa ni dhidi ya shetani, na kama isingekuwa hivyo kusingekuwa na mtu ambaye angewafuata. Nukta hii imetajwa ndani ya Quran tukufu.

Waislamu leo wanakubali kwamba dini zote za dunia kimsingi zilianzishwa kwenye ukweli hata kama hawamkubali Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Wanafurahi kuwaeleza watu wa dini zingine kwamba Islam inawakubali waanzilishi wote wa dini zao. Waislamu wengine leo wanakubali juu ya kifo cha hadhrat Issa a.s. ambayo ni sehemu ya ardhi mpya na mbingu mpya Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliyoitengeneza.

Kisha kuna mambo ambayo tunatakiwa tuyaingize kwenye matendo. Tumeshiriki kwenye utengezaji wa ardhi mpya na mbingu mpya kwa kukubali ukweli wa Ahmadiyyat na kuchukua Baiat. Sasa kushiriki kwa kweli kwenye kutengeneza ardhi mpya ni kuwa na utekelezaji. Mtume mtukufu s.a.w. alisema moyo wa mwaminio ni kama ardhi. Tuzifanye nyoyo zetu zifaidike sio kiimani tu bali kimatendo pia.

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu tumemkubali Masihi Aliyeahidiwa a.s. na sasa Mwenyezi Mungu Atusaidie kuyatekeleza mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ili ardhi ya nyoyo zetu ipate kuwa njema. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitupatia maelekezo yenye kutosha juu ya hili na sasa ni juu yetu kuyatumia.

Kuna haja ya kujitathmini sisi wenyewe. Ni jambo la msingi kwamba kila fundisho la Quran lilete mabadiliko chanya kwetu na kama ilivyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. tusonge mbele kwenye uumbaji wa ardhi mpya na mbingu mpya.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kwamba watu hupanga mipango na kuchukua hatua zote zinazotakiwa, lakini husahau maombi. Watu hutegemea sana njia za kidunia na kuyakebehi maombi. Hii ni sumu mbaya sana iliyoenea duniani kote. Akasema kwamba Mwenyezi Mungu amekusudia kuiondoa sumu hii na ni kwa sababu hiyo ameanzisha ujumbe huu wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akasema kwamba hizi ni zama za mgongano wa masuala ya kiroho. Shetani anaishambulia ngome ya Islam lakini Mwenyezi Mungu ameanzisha Ahmadiyyat ili kumshinda.

Kila Ahmadiyya analazimika kupiga hatua mbele kwa ajili ya lengo hili na kushiriki kwenye kutengeneza ardhi mpya na mbingu mpya. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema amri za Mungu ni za aina mbili. Kwanza ni kumwabudu Yeye na kutomshirikisha na kitu chochote katika dhati Yake na Zsifa zake; na pili ni kuwa na huruma kwa wanadamu, na sio wale ndugu zako wa karibu tu na wapenzi wako, bali wanadamu wote, bila kujali rangi yao wala dini yao. Mwenyezi Mungu anataka utegemee Kwake kwa yale maudhi unayofanyiwa na adui yako na sio kujilipizia kisasi mkononi mwako. Kwa kadri mtu anavyokuwa mnyenyekevu ndivyo hivyo pia zinavyokuwa kubwa radhi za Mwenyezi Mungu juu yake.

Mwenyezi Mungu Atusaidie tuweze kutimiza matarajio ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika masuala ya kiimani na kimatendo pia, na tuweze kusonga mbele katika utengenezaji wa ardhi mpya na mbingu mpya na tuwe wasaidizi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa sisi wenyewe kuwa ni sehemu ya ardhi mpya na mbingu mpya.

Meisho.

Hatari na Salama zinaowakabili Waislamu

Kutoka uk. 3

ilivyobashiriwa na Mtume s.a.w. kuwa alama ya Imam Mahdi itakuwa ni jua na mwezi kupatwa ndani ya tarehe maalum za mwezi Mtukufu wa Ramadhan (Sunan Dar Qutni).

Akiwa ni nabii wa Mwenyezi Mungu ndani ya ufuasi wa Mtume Muhammad s.a.w. (4:70), anakuwa ameitimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu (24:56), kwa kuwa kwake Khalifa aliyeteuliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu akitokea ndani ya umati wa Muhammad s.a.w. sambamba na alivyosema Mtume s.a.w. kuwa Isa bin Mariam atakuwa ni Khalifa wake ndani ya umati wake (Al muujamus swaghiir, juzu ya 1, uk. 257 kilichoandikwa na Allama Twabrani na kuchapishwa na Dar ul fikr, Beirut).

Ni Jumuiya pekee ndani ya Islamu yenye kupingana na itikadi kama ile ya watu wa Yusuf, waliodai kuwa hakuna Mtume yeyote atakayekuja baadae, itikadi imeyosemwa kuwa ni ya upotevu na yenye kumuudhi mno Mwenyezi Mungu (40:35-36).

Karibuni ndugu zetu wapenzi tuungane na Jumuiya hii iliyoanzishwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mwenyewe, ili tuiokowe dunia na maangamio na kustawisha upendo na amani duniani kote.

Jumuiya hii kwa sasa inaongozwa na Khalifa wa tano wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. anayeiongoza Jumuiya hii duniani kote kutokea London, Uingereza, nchi yenye uvumilivu na uhuru mkubwa wa kidini.

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Tanzania.

Mwisho.

Buriani Mzee Rashid Salehe wa Tabora

Na Harun Rashid Bundala
Tabora

Ilikua ni siku ya majonzi, huzuni na masikitiko mengi baada ya kupokea simu iliyopigwa na Katibu wetu wa Fedha wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ya huko Rabwah Pangale. Si mwingine ila alikuwa ni Maulidi Abdallah Kapambala aliyesema kuwa Bwana Raisi ninakufahamisha kuwa Mzee wetu Rashidi Swalehe amefariki dunia majira ya saa moja na nusu (1.30) usiku huu. Wakati nikipokea simu hiyo ilikua ni saa 3.30 usiku. ***Innalillahi wainna ilaihi rajiuun.***

Siku hiyo si nyingine ila ilikuwa ni Ijumaa sawa na tarehe 12.06.2015 ikiwa ni sawa na tarehe 25 Shaabani 1436. Kutokana na huzuni na simanzi zilizonijaa nilimjibu huyo bwana kuwa tutawasiliana kesho majira ya saa tatu asubuhi Inshaallah.

Kilichofuata ni kuanza kuwafahamisha watu wa karibu na muhimu. Nilimfahamisha Raisi wa Mkoa Mzee Abasi Kasita, Katibu wa Jamaati Tabora mjini Mwl. Dunia Yusufu, Mzee Isa Mkuyu na Yahaya Mpambije, hawa ni wajumbe wa Majlis Amila na kuwapa taarifa ya kifo cha Mzee wetu Rashidi Swalehe na kuwaomba tukutane asubuhi yake hapo msikitini majira ya kuanzia saa 2.30 mpaka 3.00 asubuhi tuangalie uwezekano wa kufika huko kwa ajili ya mazishi. Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu asubuhi ilifika na kwa pamoja tulifika kwa wakati. Kwanza tuliangalia gharama ya nauli ambayo ilikuwa ni 6,000/=, kwa mtu kwenda na kurudi ni sh. 12,000/=. Baada ya hapo ulipitishwa mchango na zilipatikana jumla ya sh. 37,000/=. Mwenyekiti wa kikao hicho Raisi wa Mkoa alimkabidhi mchango huo Raisi wa Jamaat Mzee Harun Bundala. Na baada ya hapo Raisi wa Mkoa aliteua watu wawili wa kwenda kuwakilisha Jumuiya na wanajamaat wa Tabora kwenye mazishi hayo. Wateuliwa hao ni Mzee Bundala Raisi wa Majlis Amila na Mwl. Dunia Katibu wa Jamaat. Wakati tukijadili swala hilo la msiba alitufikia mtoto wa marehemu, Abdallah akitokea Nzumbuka naye akielekea huko msibani.

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu msafara ulianza hapo saa 3.40 asubuhi kuelekea kituo cha mabasi yaendayo Sikonde. Tulifanikiwa kupata basi linaloondoka saa 4 asubuhi. Tulikata tiketi na kupanda na kuondoka saa 4.30 asubuhi na kufika Pangale kituo cha basi saa 5 ile ile asubuhi. Baada ya hapo tulipata usafiri wa kwenda huko kitongoji cha Kasekela kuliko msiba.

Baada ya kufika tulianza kutekeleza yafuatayo, kwenda kuaga mwili wa marehemu, kuandaa sanda, kumwosha marehemu, kumkafini (kuuvika sanda mwili). Wakati hayo yote yakianza kufamyika ni saa 7 mchana. Hapo saa 8.15 mchana kazi ilikamilika. Sala ya Adhuhuri na Alasiri zilisaliwa kwa pamoja. Hatimaye mwili wa marehemu uliletwa kwa kusaliwa, na baada ya sala zoezi la kwenda kumzika mzee wetu lilifanyika. Baada ya mazishi kufanyika, Mwl. Dunia alielezea uma ulioshiriki machache juu ya kifo na mazishi kwa ujumla. Na hatima yake dua ya kimyakimya ilifanyika ya kumuombea marehemu na kukamilisha zoezi zima la kuzika. Wawakilishi wa Jamaat kwenye mazishi hayo walitoa mchango wao na kumpa mfiwa bwana (mume) rambirambi yao. Baada ya hapo safari ya kurudi Tabora mjini ilifanyika.

MAISHA YA MZEE RASHIDI SWALEHE

Marehemu mzee Rashidi Swalehe alijulikana kwa jina kamili Rashidi Swalehe Mnyonga. Wa kabila la Mrangi aliyezaliwa katika Mkoa wa Singida Wilaya ya Kondoa mnamo mwaka 1924 wakiwa watatu yeye na dada zake wawili. Wa kwanza kuzaliwa akiwa mwanamke, wa pili yeye na wa tatu mwanamke. Haya ni maelezo yake aliyokuwa akinielezea wakati wa uhai wake. Kwenye mwaka wa 1934/36 akiwa na umri wa miaka 10 na 12 alifika hapa Tabora akiwa na wazazi wake na dada zake wote wawili na kufikia kijiji cha Goweko kwa ndugu wa mzee. Mzee aidha alijishughulisha na biashara, hivyo alifika hapa mjini na kuanza shughuli yake akiwa na mzee Rashidi na mkewe na kuwaacha nyuma dada zake. Katika umri huo baba alimwingiza chuo cha Kiislamu kwa ajili ya masomo ya Kuran kwa mmoja wa Mashekhe hapa Tabora. Marehemu katika masomo ya Kuran alifanya vizuri tu mpaka kuhitimu na kumaliza msahafu wote (Juzuu thelathini). Marehemu akiwa na umri wa miaka 16, Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa imepiga hodi hapa Tanganyika (Tanzania) wakati ule, hususan hapa Tabora chini ya uongozi wa marehemu Sheikh Mubarak Ahmad H.A. maulana Sheikh Mubarak katika mahubiri yake ya hapa mjini yalimuathiri sana mzee Rashidi, pamoja na kuwa na umri mdogo. ya wakati wa mwaka wa 1940 na alipenda sana kuwa karibu na Sheikh Mubarak. Mpaka ilifika hatua ya Sheikh wake kumwambia usiwasikilize hao makadiani ni makafiri. Lakini wala hakumsikiliza. Mpaka baba yake Mzee Swalehe kuingilia kati na kumuasa afuate makatazo

Mzee Rashid Saleh, enzi za Uhai wake

ya Sheikh wake, lakini naye alimfahamisha baba kuwa, ''mimi huko kwa makadiani ninajifunza sana elimu zaidi ya Tafsiri ya Kuran na Hadith za Mtume Muhammad s.a.w ambayo huko kwa masheikh wangu sijapata''. Mzee wake alimwacha aendelee. Wakati msikiti wa Alfadhil unajengwa, naye marehemu alishiriki akiwa bado kijana. Anavyoelezea ni kuwa marehemu shekhe Mubaraka alimpenda na kumwita "huyu Rashidi wangu" kati ya umri wa miaka 18 na19 alijiunga na Jumuiya na hatimae kule chuo kufutwa kabisa.

ZINGATIA

Kiamshacho mahaba, ni uzuri wa hisani,
Iguswapo ile huba, inayokaa moyoni,
Tamu ya ajabu huba, iunguzavyo moyoni,
Hapendi kiafkani, ampendaye Karima.

Maneno hayo yamo katika kitabu cha Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri. Inaonyesha wazi mzee Rashidi aliathiriwa na mafunzo hayo na hatimaye alimpenda hasa Karima.

Kwa jumla mzee alikuwa hakusoma masomo ya kizungu. Hapo ikalazimu baba yake, (Sheikh Mubarak) amtafutie kitabu cha, a e i o u, na kufundishwa kusoma hata kuandika angalau jina lake. Haya yote akawa ameweza kiasi chake. Aliendelea kuwa na Maulana mpaka walifikia hatua ya kushauriana ili aoe mke. Ushauri huu ulifika kwa baba mzazi na kukubaliwa. Panapo mwaka wa 1952 mzee Rashidi alioa mke. Kipindi hicho akiwa na umri wa miaka takriban 28. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu walijaaliwa kuzaa mtoto mmoja wa kiume na baba yake akampa jina Swalehe. Hata hivyo Maulana Sheikh Mubaraka hakumwacha hivi hivi ila kwa elimu yake ya Kuran alimpa kazi ya kuwafundisha watoto wa Kiahmadiyya, kama vile Sheikh Yusufu Kambaulaya na wenzake.

AACHA MKE

Kwenye mwaka wa 1956 mwalimu Rashidi Swalehe alirudi mara moja nyumbani kwao Kondoa alikaa huko mwezi mmoja au miwili, na hatimae alirudi na kuendelea na shughuli zake za kufudisha. Hata mimi (Bundala) alinifundisha miaka ya 1957 kabla ya kujiunga na chuo cha Ahmadiyya Dar es salaam. Hata hivyo walishindana na mke wake kwa kutojiunga na Jumuiya, hivyo aliamua kumwacha. Wakati wote huu, Maulana Sheikh Mubarak akiwa Amir na Mbashir Mkuu makao yake yakiwa Nairobi. Hata hivyo alikuwa haachi kuja Tabora alikuwa na vipindi vya kufundisha huko Tabora Boys.

Kwenye mwaka 1960 kwa fadhila za Mwenyezi Mungu alijaaliwa kuoa na kuzaa watoto 6 (sita), wa kiume watano na wa kike mmoja. Hao ni Abdalla, Shabani, Aziza, Saidi, Mashaka na Ramadhani. Kati ya hao watoto ni Shabani tu ndiye aliyefariki. Naye huyu mama alimshauri kujiunga na Jumuiya naye pia alikuwa mgumu kukubali shauri hilo. Miaka 1997 hatimaye waliachana. Mzee hakuchoka kutafuta mama mwingine. Safari hii alianza na kumhubiri baada ya kumpata. Baada ya kukubaliana, mwaka wa 1998 alioa mke, huyu mama alikuwa ni mtu mzima na ni wa kabila la Kisukuma. Hata hivyo miaka ya 2004 alifariki dunia.

Katika miaka ya 1990 baba yake mzazi alifariki na dada yake wa mwisho akafariki 1998. Na dada yake mkubwa alifariki 2006 na kubaki mzee Rashidi pekee. Mzee Rashidi baada ya kufiwa na mke aliishi pekee kwa muda na baadae miaka ya 2007 aliuza nyumba yake huko Ng'ambu alikokuwa anaishi na kwenda kukaa na mwanaye Swalehe huko maeneo ya Kiloleni Tabora. Mzee aliendelea kuwa pale kwani Swalehe alikuwa na nyumba yake hapo Kaloleni.

MZEE RASHIDI APATA PIGO

Mnamo mwaka wa 2010, mzee Rashidi alipata pigo la kufiwa na mlezi wake mwanaye bwana Swalehe na kubaki na mkamwana. Hata hivyo mzee aliyumba kimaisha kwani kuendelea kukaa na mkamwana ilikuwa ni ngumu, kwani miongoni mwa watoto wake wa mke wa pili hakupatikana mrithi wa kumrithi Swalehe wa kumlea mzee wao kwani walidai kuwa alikuwa ni mkorofi. Mzee aliyumba hasa mpaka ilifikia mtoto wake wa kike bi Aziza alikaa na kushauriana na mumewe na kukubaliana wamchukue ili waendelee kumlea. Hatimae mwaka 2012 alichukuliwa na Mkwilima huko Pangale kitongoji cha Kasekela mpaka ulipomfika umauti mwaka 2015.

Katika maisha yake yote, mzee alijitahidi kuwahubiri wanawe wote 7 (saba). Hakuna hata mmoja aliyeelekea kujiunga na Jumiuya Ahmadiyya, mpaka Mwenyezi Mungu Alipomchukua na kurudi kwa Muumba wake kwa maisha yake ya milele.

Hata hivyo mzee huyu katika maisha yake yote alishikamana na Jumuiya wala hakurudi nyuma hata siku moja. Mzee Rashidi hata hivyo alikuwa Musi. Pia tunamtakia kila la kheri katika maisha yake ya milele, Amin.

NYONGEZA

Mtu kupata heshima, ni kumcha Rahmani,

Ndipo uone salama, akhera na duniani,

Wamchao Rahmani, ndio wenye mwisho mwema.

Mwisho: Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwingi wa Ukarimu.

Bustani ya Washairi

MASHEHE MWASIKITISHA NAWAMBIA SI UTANI

Nyote muliopo sasa enyi mulowapinzani
Ambao mwamkanusha nabii wake manani
Huyo aliyetufika zama hizi duniani
Amabye kafananishwa kafanishwa na nani?
Kafananishwa na Isa wa binti wa Imraani

Ambaye ndiye hakika mrejeshaji undani
Kiroho ulotoweka halisi wa quran
Ili ipate huika upya dini ya manani
Ipate simama upya izishinde zote duniani
Umma wetu kwa hakika uondoke ujingani
Gizani upate toka urudi tena nuruni

Hivyo nawafahamisha mashehe wanazuoni
Huyo ,unomkanusha kiroho jieleweni
Nanyi mumerithi visa halisi vya makuhani
Tena wa zi mwaonesha nyinyi hasa fahamuni
Kuwa ndio ninyi hasa mulotamkwa zamani
Zama hizi kwa hakika mutapeleka motoni

Wazi wazi mwaonesha halisi hasa ni nyinyi
Ndio muliiotamkwa zama hizi duniani
Motoni mutapeleka kwa elimu za vichwani
Na ushahidi nawapa mulo nao eleweni
Ya kuwa ni ni ninyi hasa mupelekao motoni
Mabii mpya kafika huyo wa mola manani

Nabii huyo kafika nan a ushahidi rasmi
Mola alouonesha wa mbingu na ardhini
Ili kumthibitisha tuweze kumuamini
Kuwa ni nabii hasa si muongo abadani
Ni yule alotamkwa keshafika duniani
Bali munamkanusha mwapingana na manani

Nabii huyo kafika na ushahidi rasmi
Mola alouonesha wa mbinguni na ardhini
Ili kutusadikisha mola katia saini
Ni nabii hana shaka waja wangu mwaminini
Mwana Mariamu hasa ni huyo mpokeeni

Mwana mariamu hasa ni huyo mola manani
Mwenyewe kathibitisha leo wanazuoni
Wa makundi yakuzusha mwapingananan manani
Mwasema ushaisha utumewake manani
Mwishoni umeshafika huyo ni mtume gani
Munasema katakata huyo hamumuamini

Mwatisha mwasikitisha mashehe wanazuoni
Enyi muliopo sasa wa elimu ya vichwani
Mwasikitisha mwaogopesha mbaya wenu undani
Nabii mwamkanusha alotumwa duniani
Zam hizi kuhuisha upya dini ya manani
Kila hila mwapitisha watu wasimbaini

Munasema umeisha utume wake manani
Hivyo huyo alofika eti mtume wa nani?
Kumbe uongo mwazusha mkubwa uso kifani
Sababu ulioisha hasa ni utume gani?
Ni wenye sheria mpya huo ndio eleweni
Mwishoni uliofika hauletwi duniani

Lakini nawajulisha utume wake manani
Usio sharia mpya waendelea juweni
Na mola kathibitisha ho upo fahamuni
Maana huyo alofika zama hizi duniani
Alojitangaza hasa ni muhuishaji dini
Huyo munomkanusha mashehe wanazuoni

Huyo munomkanusha enyi wanazuoni
Alojitangaza tosha ni nabiiwa manani
Mola kamthibisha kwa ishara za mbinguni
Ili kutusadikisha ni kweli yake maoni
Abadani hajazusha katujulisha manani
Hivyo munomkanusha nazidi waelezeni

Enyi munomkanusha nabii huyo juweni
Kwa kusema umeisha utume wake manani
Muelewa vy kutosha elimu imewahuni
Hamunayo ninaapa ya isilamia dini
Ujinga unawatesa wa elimu ya vichwani
Uongo mwakithirisha unaotia motoni

Uongo mwakithirisha kwa elimu za vichwani
Hadithi mwazipotosha na kitabu cha manani
Undani mwabadilisha kwa fasiri za kubuni
Hivyo muelewe tosha mumezama uasini
Uasi mkubwa hasa unaosaliti dini
Musipojisahihisha kutubia kwa manani

Musipojisahihisha kutubia eleweni
Ahera mutaja juta nawambia zindukeni
Hasara itawafika kumalizia motoni
Maana hakimwapotosha mwaitia batilini
Kwa elimu za kuzusha nabii mwamfitini
Bado nasaha nawapa iwapo muujingani

Name nasaha nawapa nazidi wanasihini
Iwapo kweli hakika mashehe muujingani
Nawaapia naapa huyo musomuamini
Ni nabii hana shaka ametumwa na manani
Dini iliyotoweka ikahama umatini
Aturejeshee upya ili tutoke gizani

Hivyo nasaha nawapa mashehe wanazuoni
Enyi munomkanusha huyo muhuisha dini
Jiwahini kwa haraka tubieni tubieni
Ili apate ridhika mola awe radhi nanyi
Uradhi apate wapa awasamehe na nyinyi
Ili mupate okoka mujitowe hasarani

Ili mupate okoka mujitowe uasini
Uasi ule hakika wa ibilisi sheitani
Ambao mumerithishwa mashehe wanazuoni
Wa makundi ya kuzusha yalosemwa ya motoni
Yenye elimu za vichwa zinazopotosha dini
Tubieni kwa haraka mwombeni radhi manani

Bali nasaha nawapa mashahe tafakarini
Ili muviwache visa halisi vya makuhani
Walivyovitenda hasa kumtendea manani
Kwao vilosababisha wengi wangie motoni
Nanyi mumerithi hasa mujuwe huo undani
Tubieni kwa haraka mulobaki duniani

Viwacheni hivyo visa kiroho vya usheitani
Nanyi mulivyorithishwa halisi vya makuhani
Viongozi hasa hasa wale wakuu wa dini
Wa isiraili hasa walomuasi manani
Masihi wao kufika wakakosa muamini
Wakamtenda na visa vingi vya kumfitini

Wakatenda vingi visa kiroho kumfitini
Ambavyo mumerithishwa wasasa wanazuoni
Wanazuoni hasa ewa makundi ya motoni
Wenye elimu za vichwa zinazosaliti dini
Ambao mwanikanusha masihi8 wenu na nyinyi
Huyo aliyetufika zama hizi duniani

Ambao mwafahamishwa kuwa mumo uasini
Mahubiri munapata na tena ya kila fani
Madhumuni nanyi hasa muondoke ujingani
Nuru isharudi upya musibakie gizani
Haki sasa ishafika musibaki batilini
Bali la kusikitisha mumezidi upinzani

Hiyo ndo hatari tosha inayowakabilini
Lakusema mutakosa mbele ya mola manani
Maana munafahamishwa ili mujuwe undani
Muhuishaji kafika wa isilamia dini
Upya kaja kufundisha kitabu ch qurani
Ili kutuelimisha tuijuwe upya dini

Bali mukifahamishwa mashehe wanazuoni
Wa makundi ya kuzusha hayo yote ya motoni
Hamutaki mwakanusha munayopewa maoni
Mwamkana katakata huyo muhuisha dini
Ni kafiri munamwita hamutaki muamini
Viburi munazidisha kumtendea manani

Kila mukieleweshwa nabii mumbaini
Viburi munazidisha vya elimu ya vichwani
Kwa hivyo nawajulisha haina karaha dini
Mimi nawafamisha muzudi juwa undani
Muonyaji keshafika ametumwa na manani
Yule aliyetamkwa kuja akhera zamani

Muonyaji keshafika kutunusuru juweni
Elimu kairejesha halisi ya qurani
Dini ipate huika tuondoke ujingani
Gizani tupate toka umma urudi nuruni
Hivyo munomkanusha huyo musomuamini
Mukizidi mkanusha hiari yenu juweni

Mashehe nawajulisha huyo muhuisha dini
Kuhubiri nazidisha ni nabii wa manani
Mukizidi mkanusha hiari yenu na nyinyi
Nazidi wafamisha haina karaha dini
Litakiwalo hakika nanyi mujuwe undani
Yule nabii kafika alotamkwa zamani

Litakwalo kwa hakika nanyi mujuwe undani
Nabii yule halisa alotamkwa zamani
Alofanana na isa keshafika duniani
Hivyo mukimkanusha mashehe wanazuoni
Viburi mukizidisha vya elimu ya vichwani
Katu hamutookoka mbele ya mola manani

Bimkubwa Kombo
Ahmadiyya Muslim Jamaat, Zanzibar.

UWEZO WAKE JALALI KITONGA TUMETULIA

Asallam ilaikumu, enyi ndugu wahisani
Naanzia kwa salamu, wa Dar na mikoani
Twamshukuru Karimu, tumekaa kivulini
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Mawazo yalianzia, kikao kikawadia
Ni wapi tutaanzia, tupate pa kutulia
Busara ziliwajaa, ndipo wakafanikiwa
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Ziendee shukrani, wa mwanzoni kikaoni
Ali Mosse mawazoni, Malinda na Sultani
Masamba na Hamsini, Ame Abdallamani
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Twashukuru Wadudi, makao kutupatia
Hii kweli ni zawadi, ambayo twafurahia
Tuamke Tahajudi, maombi kuendelea
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Kweli tumejionea, Mwenyezi kutupa shani
Watu walijitolea, kusafisha maskani
Zana walizigombea, kuwe safi viwanjani
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Answallu hima hima, mapanga walichukua
Khuddamu walisimama, visiki walichimbua
Lajna hakuwa nyuma, majembe waligombea
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Sasa tupo kivulini, kweli tumejinasua
Tukiwa mkutanoni, hewa tunajipatia
Wageni wa mikoani, hali wanaisifia
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Tunzi haina mapana, mwishoni nimefikia
Tumuombe subhana, kumbi zizidi kung'aa
Atujalie Rabana, njia ya kujitolea
Uwezo wake Jalali, Kitonga tumetulia.

Rehema Fadhili, Kitonga – Dar es Salaam

Idul Fitri 2015 - Dar es Salaam, Amir Sahib ahimiza Utawa

Na Mwandishi Wetu

Akitoa hotuba kwenye sala ya ya Eidul Fitri iliyofanyika Kitonga mwaka huu 2015, Amir Sahib alisema:

Na wale wanaojitahidi kwa ajili yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia zetu . Na bila shaka Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wafanyao mema. (sura, 29 aya 70).

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye kwa fadhili na rehema zake zisizohesabika Ametujaalia sisi sote kushuhudia siku hii ya leo iitwayo Eid sawa na istilahi ya dini tukufu ya kiislamu.

Ndugu zangu wapendwa, katika mwezi mtukufu wa Ramadhani sisi sote tulijitupa kikamilifu kwenye kizingiti cha Mwenyezi Mungu huku tukionesha mfano wa kimatendo kwa kuacha hata vile vitu vilivyo halali kwa ajili ya mapenzi ya Mola wetu mtukufu. Matokeo yake ni kwamba tukafunguliwa milango ya maendeleo na mafanikio ya kiroho na kujaaliwa kufanya ibada usiku na mchana kwa furaha na tukajisafisha na kujitakasa nafsi zetu kwa matendo mema katika siku hizo chache zenye baraka nyingi za mwezi wa Ramadhani. Na hivi leo tumejumuika kuadhimisha siku kuu ya eidi ambayo ni siku ya furaha kubwa kwa kila aliyefunga saumu ya Ramadhani akiwa na imani na nia ya kupata thawabu.

Kama tujuavyo kwamba shabaha hasa ya ibada ya saumu ni kujitahidi kuzidi katika Uchamungu na kujenga uhusiano imara ulio hai na Allah ambaye Ameeleza waziwazi " ASSAUMU LII WA ANAA AJZI BEHII" yaani malipo ya saumu ya mtu ndiyo yeye Mwenyewe. Muradi wake ni kwamba yeyote atakayejaaliwa kutekeleza ibada ya saumu vizuri , atampata Mola Wake na kumpata Allah ndiyo kupata kila kitu kama Asemavyo Hazrat Ahmad as " Pepo yetu ni Mungu wetu."

Hivyo basi, maadhimisho ya siku ya leo ni kwa ajili ya kufanikiwa kumpata Mola wetu Aliyetuumba na kutujaalia kila kitu.

Khalifa Mtukufu wa pili , Hazrat Musleh Ma'uud ra akieleza maana ya eid alisema: " Siku kuu yetu ya eidi ni nini ? Ndiyo hii ya kwamba tuweze kumpata Mola wetu aliye mpendwa wetu. Mtu anayejitahidi na kuvumilia taabu, hashindwi kumpata Mola wake na anapompata Mola wake, anajisikia furaha na utulivu wa namna hii ambayo hakuna yeyote awezaye kuiondoa". Kisha alisema: "Basi shabaha ya siku kuu yetu ya Eidi ndiyo hii ya kwamba sisi tuweze kumpata Mola wetu na njia ya kumpata ni hii kwamba tutoe dhabihu kwa ajili Yake. Kama tunakumbuka shabaha hiyo basi eidi yetu ndio eidi ya kweli".

Amir Sahib, Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akigawa Tamtam kwa Atfaalul Ahmadiyya mara baada ya Sala ya Iddi.

Ndugu zangu wapenzi, leo tumepata nafasi ya kuadhimisha siku kuu ya eid baada ya kutekeleza ibada takatifu ya saumu ambayo shabaha yake hasa ni kumfanya mtu awe mcha Mungu jinsi ilivyoelezwa ndani ya Qurani Tukufu ili mpate kumcha Mungu kwani wamchao Mwenyezi mungu ndio wanaopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu kuliko watu wote kama Asemavyo ndani ya Qurani Tukufu

" Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi". (sura , 49 aya , 13)

Mtume wetu mtukufu, Muhammad saw alisema "Innallaha yuhibbu l'abda ltaqiyya ...." yaani Mwenyezi Mungu Humpenda mtu ambaye ni mcha Mungu.

Hazrat Abu Huraira ra anasimulia ya kwamba mjumbe wa Allah saw alisema: Ewe Abu Huraira, shika ucha Mungu, utakuwa mwenye ibada kuliko watu wote, uwe na tabia ya kutosheka, utakuwa mwenye shukurani kuliko watu wote, upende kwa watu unayopenda kwa ajili ya nafsi yako utakuwa mwaminio, umtendee vizuri jirani anayeishi katika ujirani wako, utakuwa mwislamu, na usicheke sana kwani kucheka sana kunaua moyo".

Hazrat Wabiswah bin Ma'bad anasimulia ya kwamba nilimwendea Mjumbe wa Allah saw naye akasema: Je umefika ili kuuliza kuhusu wema? Nikasema: Naam. Akasema: Jiulize moyo wako. Wema ndio ule unaotuliza nafsi yako na moyo wako. Na dhambi ndio ile inayotia dukuduku rohoni na kutatiza kifuani hata kama watu wakutolee fatwa ya hiyo kujuzu na kusema hiyo ndiyo sawa".

Sayidena Ahmad as, Masihi na Mahdi aliyeahidiwa alisema :

"Shikeni ucha Mungu kwani ucha Mungu ndio mzizi wa kila wema.

Maana hasa ya ucha Mungu ni kujiepusha na njia nyembamba za dhambi. Ucha Mungu ndio huu ya kwamba mtu ajiweke mbali na jambo linaloweza kuwa na hata shaka ya dhambi. Nilipokuwa ninatunga mashairi machache juu ya madhumuni ya ucha Mungu, nilifunuliwa mstari mmoja wa shairi moja nalo ni hili:

"Mzizi wa kila wema ndio ucha Mungu, Kama mzizi huu uko salama basi kila kitu kiko salama"

Katika shairi hili, mstari wa pili ni wa kiufunuo kwamba wema si wema bila ucha Mungu.

Kisha mahala pengine akielezea maana ya ucha Mungu Hazrat Ahmad as alisema: " Ucha Mungu ni huu ya kwamba mta akijiona anaelekea kwenye dhambi basi afanye maombi na mbinu ili kujiepusha nayo waila atakuwa hana elimu. Mwenyezi Mungu Ananena

Mtu yeyote anayeshika ucha Mungu, Mwenyezi Mungu Humtengenezea njia ya kuokoka katika kila taabu na shida. Kwa hakika, mcha Mungu ni yule ambaye anatumia maombi na mbinu kadiri awezavyo. Hivyo basi mtu anayeomba kwa maombi na juhudi ni mcha Mungu".

Khalifa Mtukufu V atba akiwasihi wanajumuiyya kuhusiana na kukuza ucha Mungu alisema: " Kwa kusonga mbele katika ucha Mungu na kwa kurithi pepo za Mwenyezi Mungu ni muhimu kwa kila mwahmadiyya kufahamu makamu ya Mwenyezi Mungu na mtaweza kufahamu vizuri makamu ya Mwenyezi Mungu , pindi mtakapofuata maamrisho Yake yote kwa kujitupa kikamilifu kwake".

Hivyo basi kila mmoja wetu anapaswa kujitahidi vya kutosha kujua na kufahamu makamu ya Mwenyezi Mungu ili aweze kuzidi katika ucha Mungu na hatimaye aweze kurithi pepo za Mola wake kama ielezavyo Qurani Tukufu yaani yule anayeogopa makamu ya Mola wake , atapata bustani mbili.

Khalifa Mtukufu wa nne wa Sayidna Ahmad as akiitolea ufafanuzi aya hii alisema: " Yeyote anayemcha Mwenyezi Mungu , atapata pepo ya duniani na pepo ya huko akhera. Na muradi wa pepo ya kidunia ni ile pepo iliyoashiriwa katika aya " alaa bezikrillahe tatmainnul qulubo" bila shaka kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu , mioyo hutulia".

Ndugu zangu wapendwa , eidi yetu haiwezi kuwa eidi ya kweli yenye furaha bila kumpata Mwenyezi Mungu na kumtanguliza juu ya vitu vyetu vyote kwa sababu chimbuko la baraka na rehema zote ni dhati ya Mwenyezi Mungu tu. Kwa hiyo , uhusiano na urafiki tuliojenga na Mwenyezi Mungu katika mwezi wa Ramadhani , tuulinde , tuukuze , tuuimarishe na tuudumishe mpaka pumzi yetu ya mwisho. Mwishowe namwomba Mwenyezi Mungu Atujaalie kusherehekea eidi ya kweli inayomridhisha Yeye. Amin.

Baada ya Sala ya Idi, Amir Sahib aliongoza maombi ya kimya na kisha wanajumuiya wakasalimiana, wakikumbatiana kwa furaha huku Atfaal na Nasirat wakijiburudisha kwa pipi walizopatiwa na Amir Sahib.

HAZINA ZETU

Niambie furaha ambayo Muingereza anaweza kuwa nayo ukimuonesha barua iliyoandikwa kwa mkono wa William Shakespear au John Milton. Na niambie pia furaha ambayo muhindi atakuwa nayo ukimuonesha barua aliyoiandika Tagor. Bila shaka na Mtanzania atasikia furaha na fahari kama aliwahi kuandikiana au kumuona mwandishi wetu maarufu Shaabani Robert. Bw. Shabani Gonga ni mwandishi ambaye alikuwa karibu sana na Shaaban Robert waliweza kuandikiana na kubadilishana mawazo kwa njia ya barua na kutembeleana. Nilipata bahati ya kukutana na Shaaban Gonga naye aliweza kunitatulia tatizo ambalo nilikuwa nalo kwa miaka mingi. Nilikuwa siku zote ninajiuliza kwamba 1959 ulifanyika m kutano wa washairi wote katika ukumbi wa Ahmadiyya katika msikiti wa Masjid Salaam, lakini Bw. Shaaban Robert hakuhudhuria katika mkutano huo. Jambo hili sikulipatia ufumbuzi wa haraka na ni barua ya Shaaban Robert iliyosaidia kutengua kitendawili hicho.

Al Aziz Gonga,

Barua yako imeniwasilia. Wajibu wako kuniandikia. Ahsante sana. Nimefurahi kabisa kwa mafanikio ya mkutano wenu uliokuwa majuzi huko Dar es salaam. Mmefanya moja la mambo ya maana kwa kuanzisha chama cha Washairi katika Afrika Mashariki.

Uchaguzi wenu wa Raisi kuwa Sheikh Mahamudu Hamduni (Jitukali) ni mzuri sana. Nimemwandikia barua kumshangilia katika kufanikiwa kwake. Uchaguzi wa Katibu Sheikh Kombo vile vile ni mzuri sana. Vivi hivi, hata uchaguzi wa wataalamu wale wanne waonekana kuwa umefanywa kwa maarifa mengi. Hazin wenu ni mtu ambaye namfahamu kuwa imara sana.

Nilikuwa na nia kubwa ya kuhudhuria katika hadhara yenu. Kama ujuavyo nimefanya kazi nyingi kwa kusudi ya chama hiki. Lakini kwa bahati mbaya nilitokewa na kadha iliyonichukua Uganda kumchukua mtoto wangu anayesoma huko katika skuli ya kindergaten (watoto wadogo). Niliporudi nimekuta barua yako nikaona mliyoyatengeneza mazuri sana. Mtu mmoja mwenye akili amesema kuwa waliopo ndiyo watoshao. Hii ni kweli tupu.

Sasa washairi wote wamekuwa ndugu. Haramu kudhuriana kwa ulimi na neno. Utanisalimia kila mtu anayenijua. Usiache kunikumbuka na kuniandikia kila upatapo wasaa.

Wasalamu,

Shaaban Robert
S.L.P 223
Tanga
07th April, 1959

Mshairi aandika juu ya Mshairi

Na Mahmood Hamsin Mubiru
Dar es Salaam

Umewahi kuona shughuli kwenye mzinga wa nyuki? Taswira hiyo itakupa nini kilichotokea katika harakati za kuzindua kitabu cha '*Historia ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abedi*' kilichoandikwa na mshairi Mathiasi Mnyampala.

Kukaribisha wageni, kuzambaza kadi za mwaliko, kupanga ratiba, ni kazi ambazo zilifanywa kwa ufanisi wa hali ya juu na kamati hii. Itakuwa sio kuweka chumvi hata kidogo tukieleza mchango wa Amiri Abedi Kaluta ambaye nyumbani anafahamika kama Msafiri. Kweli alikuwa msafiri katika kipindi hiki. Alizunguka huku na kule, akiwa na tabasamu usoni na hii yote ikiwa ni harakati za kuthamini na kulienzi jina la baba yake mzazi. Na hii ni zawadi kubwa mtoto ambayo anaweza kumpa mzazi wake. Mwenyezi Mungu hulipa jitihada za yule anayejitahidi na hiyo ndivyo ilivyotokea tarehe 12/3/2013 wakati umati wa watu ulipomiminika katika ukumbi wa Karimjee ili kushuhudia tukio hili la kihistoria.

Na kweli lilikuwa tukio la kihistoria katika maana nzima ya neno hilo. Dar es salaam iliyokuwa imegubikwa na jasho kali siku hiyo ilipoa na kutulia kana kwamba nayo inashiriki katika tukio hilo muhimu. Milango ya saa nne asubuhi walianza kumimika watu wenye shauku ya kutaka kujionea wenyewe tukio hilo.

Vitabu vya mabingwa hao wawili Sheikh Kaluta Amri Abeid na Mathias Mnyampala vilitandazwa mezani ndani ya ukumbi. Kulikuwa na vijana wa Varda Arts wakiwa tayari kughani mashairi ya Kiswahili. Muda wa saa nne kamili aliingia mgeni rasmi Kingunge Ngombale Mwiru na mbele kabisa walikuwepo viongozi wa dini Sheikh Tahir Mahmood Khan – Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania na viongozi wengine wa Kikristo.

Sheikh Tahir Mahmood Khan aliombwa afungue kikao hicho kwa maombi. Sheikh Tahir aliwataka kila mtu sawa na imani yake afanye maombi ya kimya kimya na katika maombi hayo akawaomba waikumbuke n chi yetu ambayo inapita katika kipindi kigumu cha mahusiano baina ya watu tofauti. Akawaomba waiombee nchi amani na utulivu wa kweli. Nae kiongozi wa Wakristo alisisitiza juu ya kujenga uelewano na kuhurumiana. Baada ya hapo ukumbi ulikuwa ni wake Kingunge Ngombale Mwiru ambaye uwezo wake wa kujieleza na kujenga hoja hautiliwi shaka na mtu yeyote. Katika hotuba yake, Kingunge alitoa wito Kiswahili kifundishwe sawasawa mashuleni kwani samaki anatakiwa akunjwe angali mbichi. Kingunge alisema kitu m uhimu katika taifa lolote ni ardhi na kinachofuata ni lugha. Bila lugha hakuna taifa. Hivyo alitaka Kiswahili kifundishwe kutoka shule ya msingi hadi Chuo kikuu. Wazo ambalo lilipokelewa kwa vifijo na nderemo pale ukumbini. Kabla ya hotuba hiyo muhimu wasomi wawili wa Kiswahili; Profesa Mugabuso Mlinzi Mlokozi alizungumzia juu ya Sheikh Kaluta Amri Abedi – Shujaa aliyesahaulika, na Profesa alizungumzia juu ya Jabali lililosahaulika Sheikh Mathias E. Mnyampala.

Yalikuwa ni maelezo ya kibingwa, kwani Profesa Mulokozi ana uzoefu mwingi kuhusu lugha ya Kiswahili bilkhusisi Mashairi.Nilipata tabu sana juu ya neno 'aliyesahaulika' hiyo ni kumhusu Sheikh Kaluta Amri Abeid. Ni kweli Sheikh Kaluta Amri Abedi amesahaulika? Au mbinu i mefanyika ya kumsahau makusudi? Na ni nani hasa wamemsahau? Haya maswali yaliendelea kunisumbua nilipokuwa

Sheikh Kaluta Amri Abedi - Mmoja wa magwiji wa sanaa ya Ushairi wa Kiswahili

nasikiliza hotuba ya Profesa Mlokozi.

Kusahau sawa na istilahi ya Islam ni jambo linalosamehewa kwani binadamu kaumbwa na sahau. Ni muhali kumlaumu mtu aliyesahau kwani hakukusudia. Sheikh Kaluta Amri Abedi hata ufanyeje ni vigumu kumsahau. Utamsahau vipi mtunzi wa kitabu kile maarufu; "Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri", utamsahauje wakati wasomi wanaendelea kunukuu maandiko hayo adhimu? Meya wa kwanza Mwafrika wa jiji la Dar es salaam utamsahau vipi? Aliyemuokoa Julius Nyerere na pigo la Kwame Nkurumah huko Cairo Misri, aliyetoa rai ya kuanzishwa jeshi la kujenga taifa, utamsahau vipi aliyemuokoa Nyerere asijiuzuru wiki chache kabla ya uhuru. Utamsahau vipi aliyebuni jina Bunge, labda unaloweza kufanya ni kujitia hamnazo, lakini ukweli ni kwamba huyo ni kiongozi ambaye sio rahisi hata kidogo kusahaulika.

Labda la kujiuliza ni nani waliomsahau? Jumuiyya ya Ahmadiyya duniani kila uchao inakumbusha kwa njia moja au nyingine wema alio utenda. Kiongozi wa Ahmadiyya duniani wa wakati huo Hadhrat Mirza Bashirudini Mahmood Ahmad (ra) alitangaza mwaka 1964 mara tu baada ya kifo cha Sheikh Kaluta Amri Abedi ya kwamba wale waliodhani Waafrika hawawezi kitu; Sheikh Kaluta Amri amebatilisha fikra hizo. Tangazo hilo lilienda dari madari. Viongozi waliofuata wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Hadhrat Mirza Nasir Ahmad, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad wameeleza mchango wa shujaa huyo katika maendeleo ya nchi yake na haya yote yametangazwa katika magazeti ya Jumuiyya ya Ahmadiyya ambayo yanapatikana katika pembe za dunia. Yupo Bwana mmoja nchini Ujerumani ambaye amempa mwanae jina la Sheikh Kaluta Amri Abedi. Katika Tanzania Jumuiyya ya Ahmadiyya imemtendea haki Sheikh Kaluta Amri Abedi kwnai kuna mwanafunzi mmoja wa Kitanzania ambaye alikuwa anasoma chuo kikuu huko Rabwa ameandika tasnif kuhusu Sheikh Kaluta Amri Abedi ambayo tasnif hiyo tayari imechapwa katika sura ya kitabu na kupewa jina la 'Almasi ya Afrika'.

Katika mikutano ya mwaka (Jalsa salana) mara kwa mara hotuba hutolewa kuhusu Sheikh Amri au mara nyingine kughani shairi lake. Kwa ujumla shujaa huyo atakuwa amesahaulika makusudi huko upande wa pili. Lakini Jumuiyya ya Ahmadiyya imeendelea kumkumbuka kwani mema ayatendayo binadamu huendelea kuishi hata mwenyewe akisha kufa.

Masjid Salaam, Shaaban Gonga na Maendeleo ya Kiswahili Tanzania

Na Mahmood Hamsin Mubiru
– Dar es salaam.

Shukrani zote ni za Allah Aliyewezesha Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya kujenga Msikiti maridadi Masjid salaam katikati ya jiji la Dar es salaam uliofunguliwa mwaka 1957. Na kwa huruma yake Allah akawezesha jumuiyya hii kutoa maana halisi ya msikiti ni nini ambao sawa na mafundisho ya Islam ni nyumba ya ibada kwa wote na ni chem chem ya elimu kwa jamii. Alhamdulillah thumma Alhamdulillah hapana shaka mwisho wa dhiki faraja, yajana sio ya leo na hucheka vizuri yule anayecheka mwishoni.

Miaka ya hamsini na sitini kuingia msikiti wa Ahmadiyya – Masjid Salaam kulihitaji ujasiri mkubwa. Kwanza kuwa tayari kutengwa, na kubugia magunia ya matusi. Kwa walio wengi haukuwa msikiti. Hayo alinieleza wakati wa uzima wake mshairi maarufu Shaabani Gonga nilipopata fursa ya kuzungumza naye Kariakoo Dar es salaam. Shaabani Gonga ni mzawa hasa wa jiji la Dar es salaam kwa maana kamili ya neno mzawa, na hivyo analifahamu fika jiji la mzizima kwa mapana na marefu. Mzawa huyo wa Dar es salaam alinieleza kuwa alifahamiana na Sheikh Kaluta Amri Abedi kutokana na usuhuba uliochimbuka kwenye mapenzi yake ya ushairi na kupigania uhuru wa nchi hii.

Akiwa Mbashiri wa Jumuiyya ya Ahmadiyya jijini Dar es salaam Sheikh Kaluta Amri Abedi alifungua milango ya Ofisi yake pale Masjid salaam kwa watu wa aina zote. Wapigania uhuru. Watafuta elimu. Wanasiasa. Washairi. Na waliotaka kujifunza Kurani Tukufu. Barua nyingi za chama cha TANU zilichapishwa Ofisini kwake. Alifungua darasa la Wabashiri wale waliopenda kujifunza Kiarabu na Kiingereza walipata msaada kutoka kwake. Aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa CCM tawi la Printi Park na Daily News Bw. Maneno Mwikuka alijifunza Kiingereza kutoka kwa Sheikh Amri Abedi.

Bwana Shaaban Gonga (Chuma) kilichomsukuma kuja Masjid Salaam licha ya woga ambao tulishaueleza hapo juu, ni mapenzi yake makubwa kwa sanaa ya ushairi. Tayari alikuwa ameshalisikia jina la Sheikh Kaluta Amri Abedi kwani alikuwa ameshasoma mashairi yake mengi katika magazeti ya "Mambo leo, Baragumu, Mhola Ziswe, pamoja na Bukya na Gandi". Na alikuwa amekwishajijengea jina kutokana na kitabu chake alichokipa anuwani ya "Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri" ambacho kilikubaliwa na wengi. Naye Mahmood Hamduni (Jitukali) mtunzi maarufu kufikia mahala pa kusema; "Umetuturufu kipenzi", na Hamisi Amani Hamisi Nyamaume kufikia hatua ya kusema; "K Amri Abedi fundi wa kwanza kutunga".

Kutokana na sifa hizo Shaaban Gonga (Chuma) alijitosa na kubisha hodi kwa Sheikh Kaluta Amri Abedi hatua hiyo ilileta tufani na lawama kubwa sana kutoka kwa marafiki zake. Marafiki zake walimshangaa sana na walianza kumkebehi na kusema ni kosa kubwa sana kuwakumbatia Waahmadiya kwa sababu kimsingi wao sio Waislam.

Aliyoyakuta kwa Sheikh Amri Abedi Kaluta yalikuwa ni kinyume na yale waliyomwambia kuwa rafiki yake hakuwa Muislam. Angalau yaliyoonekana usoni yaliweza kumhakikishia kuwa Sheikh Amri alikuwa Muislam. Kofia haikumtoka kichwani, Assalaam Alaikum ndio ilikuwa mkate wake wa kila siku, kila akimtembelea atamkuta aidha anasali au anamuomba radhi baada ya adhana kwenda kusali. Na lamsingi kuliko yote yeye alitangaza kuwa Muislam naye aliona hakuwa na haki ya kumyang'anya haki hiyo. Kilichomuudhi zaidi Shaaban Gonga ni masingizio kwamba Waahmadiyya walikuw ana adhana yao tofauti na adhana ya Waislam wengine. Jambo hili lilimzidishia hasira sana kwani kutoka nyumbani kwake aliweza kusikia adhana ya Waahmadiyya na alipofika hapa Msikitini akaisikia vizuri zaidi na akashindwa kuona tofauti baina ya adhana ya wa Ahmadiyya na Waislam wengine.

Akiwa pale Msikitini Masjid salaam jambo lililomstajaabisha Shaaban Gonga ni kwamba ofisi ya rafiki yake ilikuwa wazi takribani saa 24. Watu walikuja kuuliza juu ya Ahmadiyya, waliyoleta makala kwa ajili ya Mapenzi ya Mungu, waliokuja kushauriana kuhusu masuala ya siasa ilmuradi hakukuwa na nukta ya kupumzika utadhani mzinga wa nyuki. Na ni kweli kama alivyosema Masihi Aliyeahidiwa (as) "Muda wa Masihi hautapotezwa bure". Mwishowe Shaaban Gonga hakuwa na njia isipokuwa kuanza kusali pamoja na Waahmadiyya na hapo alizidi kugundua ukweli wa Jumuiyya hii.

Shaabani Gonga (Chuma) baadae aligundua kuwa hata wale watoto kindakindaki wa mjini pale msikitini ndipo palikuwa mahala pao pa kusoma vitabu na kubadilishana mawazo. Mmoja wa vijana hao alikuwa ni Mohammed Ali (Al Bukhri) mshairi maarufu na mwenye nasaba ndefu ya ushairi kutoka Tanga. Yeye ni kutoka katika ukoo wa Hemed Abdallah, Saidi Abdallah Al Bukhri. Hemedi Abdallah anakumbukukwa kwa utenzi wake uitwao; "Vita vya wadachi kutamalaki mlima". Kwa hakika ulikuwa ni wakati mgumu kwa wale waliojinasibisha na Ahmadiyya. Sheikh Kaluta Amri Abedi likabiliana na hali hiyo kwa hekima na busara. Husuda za watu aliziweka pembeni, akajishughulisha na kuwatumikia watu. Huduma hiyo ya Sheikh Kaluta Amri Abedi imezaa matunda; na kweli mti hujulikana kwa matunda yake uzaayo.

Ziara ya Amir Sahib Mikoa ya Kusini yafana Ashiriki Jalsa ya kanda na kuzindua Misikiti mitano

Sheikh Ali Dino Tahir –Shekh Kanda ya Kusini.Tanzania

Tunashukuru Mweyezi Mungu ametujalia kufanya Jalsa Salana ya Mikoa Mtwara na Lindi.
Kwanza kabisa tulipata taarifa ya maandalizi ya jalsa ya kanda ya kusini kuwa itafanyika hapa Masasi taarifa hiyo tuliipata mwezi wa Tano .Tulifurahi sana lakini tulikuwa na mwezi mmoja tu wa maandalizi ya jalsa hiyo na ukizingatia eneo letu lilikua chafu kabisa hivyo tukafanya maandalizi ya kulisafisha eneo letu ambapo kulitakiwa kufanyika waqar amal ya hali ya juu sana ili kupata picha kamili ya jambo lamaandalizi kwa ajili ya kiwanja cha kufanyia jalsa salana.Hivyo ilibidi tanzimu zote tushirikiane kwa pamoja ikiwa tanzimu ya lajna khudam,answarullah,at-fal kwa ujumla wake ambapo tuna tukio moja la kukumbuka at-fal moja anaye fahamika kwajina la Israfil Twahil pamoja na alikuwa mdogo lakini alijitahidi sana katika wakar amal allhamdu lillah

USAFI WA ENEO

Kwanza tulibomoa nyumba ambayo ilikuwa imebana eneo letu ambayo ilinunuliwa na jamaat na tulibomoa kwa gharama ya 130000/= kwa kuwaajili watu walio fanya kazi hiyo baada ya hapo sisi wenyewe tukaingia kusafisha kwa nguvu zetu sawa na taanzimu zetu ambapo tumeokoa zaidi ya Tsh 300000/= kwani tulifikilia kuchukua greda tulivyoona gharama ni juu tukaamua kufanya sisi wenyewe tukishirikiana na jamaati za jirani kama vile NANJOTA,MKARAKATE NA HATA LULINDI pia kwa ujumla wake tuka fanikwa katika hilo.

KUJENGA FENSI/UZIO

Ilitakiwa kujenga fensi katika eneo letu la kufanyia jalsa hapo ilitakiwa nguvu kubwa kwa jambo hilo kwani kulitakiwa miti malaumu isiyo pungua 120 na kila mti mmoja uligharimu 4000/= ambayo ni sawa na Tsh 480000/= lakini tulipata kwa kutumia trekta ya mwana jumuiyya kwa kutia mafuta na kuwalipa wachanaji wa miti hiyo na tukaipata kwa uharaka miti hiyo .pia ikatakiwa mianzi 3500 kwaajiliya kuzungushia uzio huo nakila mwanzi mmoja ni Tsh 142/=kutoka huko kijijini kwa mianzi hiyo ilitughalimu Tsh 500000/= na usafilri 100000/= kwaajili ya mafuta ya trekta kuitoa huko polini kasha tukaichana kwa nguvu zetu wenyewe na kuanza kujenga uzio wetu kwa kushirikiana mpaka mwisho tuka kamilisha hilo sawa na muda Allahamdulillah.

Amir Sahib, Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akizindua Msikiti wa Masjid Mahd - Nyangao mkoa wa Lindi wakati wa ziara yake ya mikoa ya Kanda ya Kusini hivi karibuni.

MAPOKEZI YA MGENI RASMI

Tarehe 05/06/2015 jioni tulimpokea Amir Sahib Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhri Sahib akiongozana na mashekh wawili Sheikh Ali Dino Tahir mwenyeji wake ambaye ni sheikh wa mikoa wa Mtwara na Lindi pamoja na sheikh Mohammad Afzal Batti wa Tanga .Ujio wa Amir Sahib na msafara wake ulizidi kuamsha ghera ya wana jamaat kwa kumuona Amir na Kiongozi wao kwa wale waliofika mapema kwenye jalsa .Tuliupokea kwauzuri msafara wa Amir Sahib na baada ya sala ya magharib walipata chakula cha jioni .Na asubuhi ya 06/06/2015 jalsa yetu ikaanza rasmi kwa hutuba mbalimbali zilizo himalisha nyoyo za waahamadiyya walio hudhuria katika jalsa hiyo na kuwapa simanzi wageni wetu ambo si wa ahmadiya .Natulifarijika kwa kupata hutuba ya Amir Sahib hususani pale Amir alipozungumzia maana halisi ya jihadi sawa na mafundisho ya kiisalam na wageni maalum wali vutika sana na hutuba hiyo.

TAARIFA MAALUMU

Watu 590 walihudhuria katika jalsa salana hiyo.Ambapo wageni maalumu walikuwa 15, wageni wa nje ya ahmadiya 105,na upande wakina mama walikuwa 50 kutoka jamaat mbaimbali .Na kwa baraka za jalsa hiyo tulipata baiyat 22 na tunatarajia kupata baiyat zaidi katika mwezi wa saba inshaallah kama matunda ya jalsa yetu.Na tarehe 09/06/2015 Amir Sahib alifanya zihara ya kumtembelea mmoja kati wanajamaat waliojiunga kutokana na jalsa hiyo nyumbani kwake .naye akafurahi sana kwa kutembelewa na Amir Sahib
Kwa ujumla jalsa ilienda vizuri na wana jamaat walifurahi kwa ujio wa Amir Sahib na wanajamaat wanaamini kuwa tukipata fursa hii kwa mara nyingine hali itakuwa bora zaidi na mafanikio makubwa zaidi.

بسم الله الرحمن الرحيم

Tarehe 8 Mei 2015

UJUMBE MAALUM KUTOKA KWA HADHRAT KHALIFATUL MASIH, KWA AJILI YA IJTMAA YA TAIFA YA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA NA ATFAL-UL-AHMADIYYA TANZANIA, JUNI 2015

Enyi matawi mabichi yaliyobarikiwa ya mti wa Masih Aliyeahidiwa (a.s).

Assalamu alaikum Warahmatullah Wabarakatuh.

Katika Ijtmaa zetu zote tunafanya ahadi ya kwamba tutashikamana na kila zuri ambalo Khalifa anatuamuru, lakini wakati mwingine hatumtii Khalifa hata kama anapotukumbusha kuhusu mafundisho ya Quran tukufu. Nimesisitiza mara nyingi ya kwamba kusali sala tano ni lazima, lakini bado wengine wanalisahau hili.
Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema; "kuchukua baiati yangu hakuna maana yoyote kama hakuambatani na vitendo vizuri. Ni afadhali Kama uhai wenu na kifo chenu, kila kitendo chenu na hatua yenu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee na kama katika kila udhia na dhiki (shida na taabu) hamumjaribu Mwenyezi Mungu, wala hamkati maungano yenu naye, na katika majaribu haya yote mnapiga hatua kumuelekea Mwenyezi Mungu, basi ninasema kwa hakika ya kwamba mtakuwa wateule wa Mwenyezi Mungu. Ruhusuni utukufu wa Mwenyezi Mungu uote mizizi katika nyoyo zenu na muutambue umoja wa Mwenyezi Mungu siyo tu kwa ndimi zenu lakini pia kwa matendo yenu, ili kwamba Mwenyezi Mungu pia aonyeshe kwenu kwa vitendo rehema na huruma yake. Jiepusheni na kila uovu na watendeeni binadamu kwa huruma ya kweli. Ishikeni kila njia ya utawa na uchamungu kwa kuwa hamjui katika njia ipi miongoni mwake mtakubaliwa?"
Na kwa Atfal miongoni mwenu, siku zote ninawahimiza kusema kweli daima, kutosema uongo hata kwa dhihaka, Kusoma kwa bidii, kuwa raia bora wa nchi yenu, Kusoma Quran tukufu na kudumu katika sala kila siku.
Mwenyezi Mungu atubariki sote kuwa watumishi wa kweli wa ukhalifa wa kiaahmadiyya, na atusaidie kuendelea mbele katika utii wetu na ibada zetu ili kwamba daima tupate baraka za ukhalifa na tuzidi katika vitendo vizuri na kushikamana na kamba ya Mwenyezi Mungu. Amin

Imesainiwa
Mirza Masroor Ahmad
Khalifatul Masih V

Alama za kumtambua Imam Mahdi

Kutoka uk. 12

lake litakuwa ni Ahmad, na (hilo ndio) kundi litakalokuwa na Isa bin Mariam. (An Najmuth thaaqib, jal.2, uk 41-42).

Na kuna Hadithi nyingine iliyosimuliwa na Hadhrat Hudhaifa bin Yaman r.a. aliyesema: Sami'itu Rasuulal Laahi s.a.w. wa zabaral Mahdiyya ismuhuu Ahmad wa Abdullaahi wal Mahdiyyu yaani nilimsikia Mtume wa Allah (s.a.w.) akimuongelea Mahdi ambaye jina lake ni Ahmad na Abdullah na Mahdi, (Bihaarul Anwaar, jal. 13, uk 174).

Ndani ya Kurani Tukufu, Sura ya 61:7 – 8, Mwenyezi Mungu Amemnukuu nabii Isa a.s. akitoa bishara ya kuja kwa mtume baadae ambaye jina lake litakuwa ni Ahmad na waislamu watamuona amepotoka na kwenda nje ya Uislamu kwa kudai kwake unabii, ingawa atakuwa na ishara zilizo wazi, na watamuita arudi katika Uislamu, pale Aliposema:

Na kumbukeni aliposema Isa mwana wa Mariamu, enyi wana wa Israeli! Mimi ni mtume wa Allah kwenu, nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kukupasheni habari ya mtume atakayekuja baada yangu ambaye jina lake litakuwa ni Ahmad. Alipowafikia kwa ishara zilizo wazi wakasema; 'Huu ni udanganyifu ulio dhahiri; na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye Allah uowongo na hali yeye anaitwa kwenye Uislamu, na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wadhalimu. Hizi ni kauli za Masheikh na maulamaa wa kiislamu wenye kumkufurisha nabii huyo Ahmad na kumuona ametoka nje ya Uislamu.

Ndani ya ukurasa wa 363 wa kitabu cha Hujajul Kiraama, mmeandikwa kwamba: Wakati Imam huyo aliyeahidiwa atakapodhihiri kuja kuihuisha sunna ya Mtume s.a.w. na kuzifuta bidaa, basi masheikh na maulamaa wa kiislamu watamkufurisha na kumsema kuwa mtu huyu amekuja kuiharibu dini.

Akiwasuta kwa shutuma zao hizi dhidi ya mtume Ahmad wanayemdhani kuwa ametoka nje ya Uislamu, Allah Anasema:

Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu (aliyokuja nayo Ahmad) kwa vinywa vyao, na Allah Ataitimiza nuru yake (hiyo) hata kama makafiri hao (wanaomkufurisha mtume Ahmad a.s.) wakirihike.

Yeye Ndiye Aliyemtuma mtume Wake (huyo Ahmad anayekufurishwa na waislamu wote) kwa mwongozo na kwa dini ya haki (Islam) ili aishindishe juu ya dini zingine zote hata kama washirikina (wote wanaompinga) wakirihike.

Maelezo ya aya hii yaliyomo ndani ya kitabu cha Waislamu wa sunni kiitwacho Tafsir Ibnu Jarir yanasema kwamba: Ushindi huu (wa Islamu kuzishinda dini zingine zote) utatokeaa wakati wa ujaji wa Mahdi.

Na maelezo yaliyomo ndani ya kitabu cha Waislamu wa Shia kiitwacho Bihaarul Anwaar yanasema: Aya hii iliteremka kumhusu Al Qaaim (yaani Imam Mahdi).

Maelezo ya aya hii yaliyomo ndani ya jalada la 2 la ukurasa wa 123 wa kitabu cha Mashia cha Ghayatul Maqsud yanasema: Mtume aliyetajwa katika aya hii ni Imam Mahdi.

Ndani ya Tafsir Ibun Jarir jal. 15 uk. 72 imeandikwa kwamba hali hiyo itatokea atakapodhihiri Isa.

Ndani ya Abu Daud Jal. 2 uk 216 mna maelezo haya kwamba: Katika zama za Masihi Aliyeahidiwa, Allah Atazihilikisha mila zote na kuistawisha tu Islam.

Halikadhalika jalada la 29 la Tafsiri ya Jaamiul Bayan inasema: ushindi huu utatokea wakati wa kushuka Isa mwana wa Mariam.

Maelezo haya yote yanathibitisha kuwa huyo mtume Ahmad aliyetajwa hapo nyuma si mwingine ila ni Imam Mahdi wa zama zetu hizi aliyedhihiri kwa dhati ya mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., jina lake hasa likiwa ni Ahmad na Mirza na Ghulam yakiwa ni majina ya ukoo yaliyomilikiwa pia na baba yake na hali kadhalika kaka yake kwa wakati mmoja.

Isa bin Mariam anayesubiriwa kuja ni mtu mwingine tofauti na yule Isa bin Mariam aliyetumwa kwa wana wa Israeli miaka 2000 iliyopita. Kurani Tukufu yatuthibitishia hayo kwa kutuambia: Walammaa dhuriba bnu Maryama mathalan idhaa qawmuka minhu yaswidduuna yaani anapotajwa mwana wa Mariamu kwa namna ya mfano, ndipo watu wako wanaupigia kelele (43:58).

Ndani ya sahihi Bukhari kuna ndotombilitofautializoonyeshwa Mtume s.a.w. ambamo katika kila ndoto alimuona Isa bin Mariam akiwa katika umbile na zama tofauti. Ndani ya Bukhari Kitabul Anbiyaa bab wadhkur fil kitaabi Maryama Mtume s.a.w. alionyeshwa Isa bin Maryam akiwa pamoja na manabii waliopita zamani, yaani Musa a.s. na Ibrahim a.s., na Isa huyo alikuwa na rangi ya wekundu wekundu na nywele zilizojiviringa (Curly).

Ndani ya kitabu hicho hicho cha Bukhari Babu dhikrid Dajjaali, Kitaabullibaas babu ja'adi Mtume s.a.w. alisimulia njozi nyingine ambamo alionyeshwa Isa bin Mariam akiwa na Masihud Dajjaal aliyetabiriwa kufika katika siku zetu hizi za mwisho. Isa huyo rangi yake ikiwa si nyekundu, bali ya ngano na nywele zake sio zilizojiviringa bali zilizonyooka. Hadithi hizi zilizomo ndani ya Bukhari zathibitisha kwamba Isa yule aliyepita zamani na Isa atakayekuja baadae ni watu wawili tofauti wenye maumbile tofauti.

Ndani ya Kitabu cha Hadithi cha Abu Daud, Kitabul Mahdi, Hadithi No. 7 Mtume s.a.w. alisema kuwa kipaji cha uso cha Imam Mahdi kitakuwa kipana na atakuwa na pua iliyonyooka.

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alikuwa ni wa rangi ya ngano na nywele zake zilikuwa zilizonyooka kama hadithi hiyo ya Bukhari ilivyobainisha na hali kadhalika kipaji cha uso wake kilikuwa kipana na pua yake ilikuwa imenyooka kama imevyobainishwa ndani ya Hadithi hii ya Abu Daud.

Ndani ya Tafsir 'Araaisul Bayaan jal. 1 uk. 262 chapa ya Naulkishor kuna bishara isemayo:

yaani kushuka kwa Masihi Isa bin Mariam katika siku za mwisho ni lazima kuwe kwa mwili wa mtu mwingine.

Mwanazuoni mwingine anayeafikiana na haya ni Imam Sirajud din ibnul Wardi ambaye aliandika ndani ya ukurasa wa 214 wa kitabu chake maarufu kiitwacho Khariidatul 'ajaaib wa fariidatur raghaaib kwamba:

Kuna kundi fulani limesema kwamba kushuka kwa Isa mradi wake ni kudhihiri kwa mtu fulani anayefanana na Hadhrat Isa a.s. kwa fadhili na heshima.

Akielezea makamu ya Imam Mahdi, Hadhrat Muhiyuddin ibun Arabi ameandika kwenye ukurasa wa 35 wa Sharah Fususul Hakam kwamba:

Kwa hakika, Mahdi yule atakayedhihiri mnamo siku za mwisho atakuwa ni ambaye manabii wote watamfuata katika elimu na maarifa, kwa sababu moyo wake utakuwa ni moyo wa Muhammad s.a.w. na sehemu nyingine imesemwa batini yake itakuwa ndio batini ya Muhammad s.a.w.

Rai hii haiachani na kauli hii ya Mwenyezi Mungu isemayo: Na kumbukeni Mwenyezi Mungu Aliposhika ahadi na manabii kwamba Nikisha wapeni Kitabu na Hekima, kisha awafikieni Mtume msadikishaji wa yaliyo pamoja nanyi, basi ni wajibu wenu kumuamini na kumsaidia (3:82). Yaani walishika ahadi, kwa niaba ya watu wao, ya kumuamini na kumsaidia Mtume atakayedhihiri baada ya Mwenyezi Mungu kukikamilisha kitabu cha sheria walizokuwa wakizipokea manabii, hatua kwa hatua, toka kwa Mwenyezi Mungu, zilizokuja kukamilikia kwa Mtume Muhammad s.a.w. ambaye alitoa bishara ya kudhihiri Masihi Aliyeahidiwa katika siku za mwisho wa dunia. Huo ulikuwa ni ujumbe kwa watu wa dini zote watakaokuwa wakijinasibisha na mitume wa Mwenyezi Mungu kutekeleza ahadi za mitume wao walizoshikiana na Allah, kwa kumuamini na kumsaidia Masihi Aliyeahidiwa, waila watakuwa wamefarakana na Mitume wa Mungu wanaojinasibisha nao. Na ndio sababu zinapatikana bishara ndani ya vitabu vyao vitakatifu za kudhihiri kwa manabii wao mnamo siku zetu hizi za mwisho.

Siku moja Mtume s.a.w. alisema kwamba Imam Mahdi atatokea katika eneo liitwalo Kaadiah (Qadian). Hii Hadithi yapatikana ndani ya kitabu kilichoandikwa mnamo mwaka wa 840 Hijriyya, yaani zaidi ya karne tatu kabla ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, kiitwacho Jawaahirul Asraar cha Hadhrat Sheikh Ali Hamza bin Ali Malik Twausii isemayo;

Yaani imeandikwa ndani ya Arbain kwamba kudhihiri kwa Mahdi kutatokea katika eneo la Kaadiah, Mtume s.a.w. alisema Mahdi atatokea katika eneo litakaloitwa Kaadiah na Mwenyezi Mungu Atamsadikisha na atawakusanya masahaba zake wa nchi za mbali katika idadi ya watu wa Badri, watu mia tatu kumi na tatu.

Ndani ya kitabu kitakatifu cha dini ya Kihindu cha Athar ved, kand ya 20, saukat ya 97, mantar ya 3, kuna bishara isemayo kwamba kuna mtakatifu fulani atadhihiri na kuonyesha ushujaa wake katika sehemu iitwayo Qadun.

Halikadhalika ndani ya kitabu cha Masingasinga cha Janam Saaki bhai bhala waali waddii saaki uk. 251 kuna riwaya isemayo kwamba Bwana Mardane alimuuliza hivi Guru Nanak: Guru sahib! Je kutakuwepo na Guru mwingine atakayekuwa mtakatifu zaidi kuliko Kabir Bhagat? Kama atakuwepo ni wapi na lini? Hapo Guru Nanak akasema Guru ajaye atakuja miaka 100 baada yetu, atakuwa ni mmiliki wa ardhi na atatokea katika maeneo ya Batala. Qadian imo ndani ya eneo miliki la Batala.

Kitabu cha Wahindu cha Athar Ved, kand ya 20, saukat 115, mantar 1 pia kinatoa bishara ya mtakatifu mmoja atakayedhihiri ambaye jina lake litakuwa ni Ahmad pale kiliposema;

Ahmad hii pitushpirii, maydhaa mirii, tas yaa jagar bih aham, suriya ruwaa jinii

yaani ni Ahmad huyo huyo kwa hakika ndiye atakayeushika ukweli ulioletwa na baba yake wa kiroho (s.a.w.), naye atasema hivi: Enyi watu! mimi nimeumbwa kama jua kati yenu kwa ajili ya ukweli huu, nami ninaziremba kauli zangu kwa elimu ya baba yangu wa kiroho, ambaye kwaye mimi binafsi hupata nguvu.

Walii na mwanazuoni maarufu wa Kiislamu aliyepita miaka mingi sana kabla ya kunzishwa Jumuiya ya Ahmadiyya, Hadhrat Mulla Ali Qaari r.a., ameandika ndani ya Sharah Mishkaat uk. 348 akiisherehesha ile Hadithi mashuhuri ya madhehebu 73 anasema:

Yaani basi hayo madhehebu 72, yote yatakuwa ya motoni, na dhehebu litakalookoka litakuwa ni la watu wa suna zilizotakasika za kiMuhammad na njia takatifu ya kiAhmadiyya.

JALSA SALANA TANZANIA 2015

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry anapenda kuwatangazia Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika kwenye siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 02, 03 na 04 Oktoba 2015, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah.

Wanajumuiya wote wanaombwa wajitahidi ili wasikose kuhudhuria Jalsa hiyo.

Aidha Masheikh, Marais na Walimu wa mikoa na matawi yote nchini wanaagizwa kujitahidi kuwahimiza wanajumuiya kuhudhuria kwenye Jalsa hiyo.

Misikiti mitatu yazinduliwa

Kutoka uk. 12

kundi hili walikuwemo pia waandishi wawili wa habari ambao walirikodi vipindi vya Jalsa kwa kamera zao na wakasema watavirusha kwenye TV za nchini mwao watakaporudi nyumbani.
Mgeni mmoja alisema, muda wote alikuwa akitafakari sana juu ya mkusanyiko huo mkubwa wa Jalsa na akasema hata nchi kubwa zilizoendelea haziwezi kuandaa kitu kama Jalsa. Mgeni mwingine alisema ndio mara ya kwazna maishani mwake kukutana na watu wema waliokaa pamoja. Mtu huyo alivutiwa sana na ujumbe wa Islam na kusema Waahmadiyya wanatekeleza kwa matendo yale yote yaliyowekwa kwenye ujumbe wa maandisho ndani ya mabango.
Mwandishi mmoja wa habari kutoka Macedonia alisema ameshawahi kuzunguka sehemu kadhaa za dunia kwenye mikutano mbalimbali lakini kati ya hiyo yote ameona Jalsa ni mkutano bora kabisa kushinda yote aliyowahi kuhudhuria. Alivutiwa sana na mazingira yote ya kuvumiliana na udugu yaliyoonekana wakati wote wa Jalsa.
Mgeni mwingine alisema hii ni mara yake ya kwanza kufika kwenye Jalsa na alifuatilia hotuba zote kwa umakini. Alisema kabla hakuwa na wazo kwamba ndani ya Islam kuna Jumuiya kama hii, lakini sasa ameitambua na kuonja ladha ya Ahmadiyyat na anajisikia kuwa miongoni mwao.
Mgeni mwingine alisema ataendelea kuyatafakari yote aliyoyasikia kwenye Jalsa na hasa ataendelea kutafakari zaidi juu ya tofauti baina ya Waahmadiyya na Waislamu wengine. Akawa na wazo kwamba Jumuiya ijitahidi kutuma Mbashiri kila sehemu ambapo hakuna Mbashiri wake.
Mgeni mwingine alisema hatimae kwa mara ya kwanza kwenye maisha yake ameweza kuelezwa kuhusu Islam kupitia Jalsa na amesikiliza hotuba zote kwa makini sana.
Mgeni mmoja kutoka Bosnia alisema: Hakuwa na ukaribu mkubwa na jamaat hapo kabla lakini baada ya kukutana na Hazrat Khalifatul Masih sasa anajisikia kuwa karibu zaidi na jamaat na heshima yake kwa Huzoor imeongezeka sana.
Familia moja ya Kirashia ilikuja ikitokea Sweden wakifuatana na mwanajumuiya mmoja mpya. Ndugu huyo alijiunga na Jumuiya mwaka 2013 lakini hakuwa amekutana na Hazrat Khalifatul Masih. Baada ya kukutana na Huzoor alikuwa mwenye jazba sana. Alikuwa na tatizo la mguu na muda wote wa safari ambapo alikuwa akiendesha gari ilimbidi kupumzika kila baada ya masaa mawili ili kunyoosha mguu wake. Ingawaje baada ya kurudi aliwasiliana na Huzur kwamba hakupata tatizo lolote na hakukuwa na haja ya kusimama hata mara moja njiani na akainasibisha hali hiyo na baraka za Jalsa.
Mama mmoja kutokea Croatia alisema alishawahi kusoma moja ya kitabu cha Kiongozi wa Ahmadiyya na pia alishasikiliza hotuba yake ya Peace Symposiums 2014/2015. Akasema alidhani kwamba atakuwa ni mtu mkali sana lakini baada ya kukutana naye amejionea kwamba ni mtu mpole sana.
Mgeni mwingine kutokea Hungary alisema alivutiwa sana ni jinsi kila mtu, watoto, vijana na wakubwa kila mmoja anavyomsalimia mwenzake kwa moyo wote katika Jalsa. Ingawaje hajui lugha ambazo watu hawa walikuwa wakiongea lakini nyuso zao wote zilikuwa zikionesha kwamba ni watu wenye hisia kali za mapenzi. Alisema ameshawahi kusafiri magharibi na mashariki ya dunia lakini hajawahipo hata mara moja kuona kama aliyoyaona kwenye Jalsa.
Mgeni mwingine kutoka Hungary ambaye kiimani ni Jew (Myahudi), alikuwa mgumu mgumu alipokuwa akiongea na Mbashiri wetu kabla ya kuja kwenye Jalsa. Lakini baada ya kukutana na Huzoor akasema kwamba sio tu Waahmadiyya wanaamini juu ya Mapenzi kwa Wote chuki si kwa yeyote bali kwa hakika wanaishi sawa na usemi huo. Pia ameahidi kutoa msaada utakaohitajika na Jamaat huko Hungary.
Mgeni mwingine kutokea Hungary ambaye kwa asili ni mzaliwa wa Burkina Faso alikuja kwenye Jalsa na binti zake. Mke wake ni Mhangary na hivyo hakupenda binti zao wafuatane tu na baba yao peke yao na hivyo akamuomba mama yake (bibi ya watoto wake) afuatane nao. Bibi yao huyo alivutiwa sana na Jalsa kiasi hiki kwamba naye akaazima mtandio na kuanza kuvaa. Walipokutana na Hazrat Khalifatul Masih alikuwa mwenye jazba sana na akasema dunia ya Ahmadiyyat na Jalsa ni ulimwengu tofauti kabisa kwa namna zote zilizo nzuri.
Mgeni mmoja kutoka Ujerumani ambaye naye kwa asili anatokea Central African Republic (Afrika ya kati) alisema wakati alipoalikwa kwenye Jalsa alidhani angalau kunaweza kuwa na wageni kama mia hivi. Lakini alipohudhuria mawazo yake hayo yakawa si sahihi na akajikutia kama yuko kwenye nchi ya kipekee.
Mgeni mwingine kutoka Montego alisema alisikiliza hotuba zote na kufuatilia mipango yote na ameiona kuwa na ubora wa kipekee. Mgeni mwingine kutoka Montego alisema Waislamu husema - Mungu Apishe mbali - kwamba Waahmadiyya hawamwamini Mtukufu Mtume s.a.w.. Ingawaje kwa jinsi alivyosikiliza hotuba za kwenye Jalsa kwa umakini mkubwa na kushuhudia kwa macho yake amegundua kwamba tuhuma hizo ni uongo mtupu.
Mgeni mwingine kutoka Belgium ambaye kwa asili ni Mmorocco alisema mwanga wa kiroho kwenye Jalsa uliibadilisha roho yake yote. Alisema kwa kumsikiliza Hazrat Khalifatul Masih mtazamo wake juu ya Jamaat umebadilika na akaomba Mwenyezi Mungu amsaidie ili aweze kufanya Baiat.
Mgeni mwingine kutoka Ujerumani alisema hii ni mara yake ya kwanza kuhudhuria Jalsa na amepata nafasi ya kuielewa kwa mara ya kwanza Ahmadiyyat. Akasema kila alichokisema Hazrat Khalifatul Masih ni kweli tupu na kama watu watekeleze yale anayowaongoza basi dunia ingekuwa ni makazi ya amani.
Mwanajumuiya mpya kutoka Ufaransa ambaye amefanya Baiat wiki tatu zilizopita, alisema siku zote alikuwa ni mwislamu lakini hakuwa na umadhubuti kwenye imani. Wakati aliposali sala yake ya kwanza nyuma ya Huzur alianza kububujikwa na machozi. Alisema tangu ajiunge na Ahmadiyyat kila siku anapata Ishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
Mgeni mwingine ambaye ni Mwanafunzi alisema kabla ya kuja kwenye Jalsa alikuwa na mtazamo hasi kabisa juu ya Islam ukiwa ni mtazamo ambao ameupata kupitia vyombo vya habari, lakini baada ya kuhudhuria Jalsa amegundua kwamba kila kitu ni tofauti na chenye mwelekeo chanya. Akasema kwamba amegundua Uislamu wa kweli kwa Waahmadiyya.
Mgeni mwingine kutoka Lithuania ambaye ni mwanasheria amevutiwa sana na Jalsa. Alisikiliza hotuba zote za Hazrat Khalifatul Masih na anajisikia kwamba amefika kwenye Jalsa kwa ajili ya kuujua Uislamu wa kweli. Akaahidi kujitolea huduma za kisheria na masaada wowote Jamaat utakaouhitaji huko Lithuania.
Mgeni kutoka Bosnia alisema Hazrat Khalifatul Masih anamuelezea Mungu Aliye hai. Alisema leo ni Jamaat Ahmadiyya pekee isemayo kwamba Mungu yuko hai kama alivyokuwa zama zote.
Mgeni mwingine aishie mipakani mwa Ujerumani na Belgium alisema kabla ya kuja kwenye Jalsa hakuichukulia dini kuwa ni jambo la kutiliwa maanani. Lakini baada ya kuhudhuria Jalsa mawazo yake yamebadilika.
Mgeni mwingine ambaye alifanya baiat baada ya kuguswa sana na hotuba ya Kiigereza ya Hazrat Khalifatul Masih; alisema sasa moyo wake umejaa mapenzi na mwanga.
Mgeni mwingine kutoka Syria ambaye baba yake alikuwa ni Ahmadiyya na alishamfanyia Tabligh lakini mtoto huyu akawa hajafanya Baiat. Alishawahi pia kuwa na kipindi cha maswali na majibu na Mbashiri wetu lakini hakuwa ametosheka. Aliombwa kufanya maombi na akasema aliomba kiasi fulani, kisha akaambiwa ajitahidi kuweka mkazo zaidi kwenye maombi. Kwenye siku ya pili ya Jalsa alikuwa na mkutano na Hazrat Khalifatul Masih baada ya hotuba yake. Mgeni huyu alimwambia Mbashiri wetu siku hiyo ampatiye hoja moja ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kutoka kwenye Quran Tukufu ambayo alimpatia na pia akamweleza baadhi ya bishara za Masihi Aliyeahidiwa a.s. na jinsi zilivyotimia. Mgeni huyu alikuwa tayari kufanya baiat kwani alishapata ushahidi alioutaka. Usiku ule pia alifanya sana maombi na akapata njozi. Kwenye njozi aliona maandishi makubwa yameandikwa ukutani Al Ahmadiyya. Wakati wa hotuba ya Huzur akatamani kama angekuwa karibu sana na Huzur. Muda mfupi akapata usingizi na akajiona amekaa mbele karibu sana na Huzur. Jambo hili lilimridhisha sana na akafanya Baiat.
Mgeni mmoja Mkristo kutokea Italy alikuja kwenye Jalsa. Huko Italy yeye ni katibu Mkuu wa taasisi moja iitwayo 'Religions for Peace.' Pia anao uenyeji huko Vatican. Alishiriki kwenye Jalsa kwa mtazamo chanya sana na baadae akaandika makala ambapo alisema analazimika kukiri kwamba ameguswa sana na yale aliyoyaona. Akasema Waahmadiyya ni waislamu wa ukweli. Akasema pia ni jambo alilojionea mwenyewe kwamba watu kwa maelfu wakiwa wenye asili mbalimbali wamehudhuria kwenye Jalsa wakati wahudumu walikuwa ni mia chache tu. Akasema mtu mmoja aliyekuwa akimuendesha alimwambia amechukua likizo ya wiki mbili bila malipo ili aweze kujitolea kwenye Jalsa. Kuhusu hotuba ya Hazrat Khalifatul Masih alisema inaongoza kwenye njia iliyo sawa.
Mgeni mmoja kutoka Syria alisema kabla ya hapo hajawahipo kuona hafla yoyote iliyopangwa vyema kushinda Jalsa. Akasema pia ameshawahi kusoma Baraheen e Ahmadiyya na anayo imani kwamba hakuna mwanaulamaa yeyote kwenye karne ya kumi na tisa aliyeweza kuandika kitabu kama hicho katika kuutetea Uislamu.
Kwa kwaida wageni huwa hawaoneshi mapungufu wakati wa Jalsa, lakini wageni wawili, akinamama kutoka Albania walisema kwamba kwa upande wa kinamama chakula kingi sana kinapotezwa. Uongozi wa Jalsa, hasa upande wa kinamama ulitilie maanani jambo hili siku zijazo. Mama mmoja, mgeni kutoka Macedonia alilalamika kwamba makazi yao yalikuwa mbali sana kutoka sehemu ya Jalsa na ilikuwa ni jambo linalochosha kwenda na kurudi huko. Uongozi pia ujitahidi kuandaa makazi ya karibu kwa watu kama hao. Afisa Jalsa mwenyewe pia aliorodhesha baadhi ya mapungufu. Na hivi ndivyo ifaavyo zaidi kwamba mtu aone mapungufu yake kwani inakuwa rahisi zaidi kuyaboresha. Alisema msisitizo zaidi unahitaji kuwekwa juu ya usafi. Baadhi ya watu pia inasemwa walilalamika kwamba kwenye orodha ya vyakula hakukuwa na jamii ya tambi. Ikumbukwe kwamba lengo kuu la Jalsa ni kupata chakula cha kiroho na juu ya chakula cha kimwili, chochote kitakachotayarishwa tujitahidi kukitumia hicho bila ya malalamiko. Baadhi ya wakati wahudumu huchukua msimamo mgumu na mkali ambao huwaumiza baadhi ya watu. Wafanyakazi wapime alama za mazingira, wakiona kwamba kweli mgeni anayo dharura iliyo ya msingi, basi wasishikilie tu kanuni zilizopangwa, bali wamsaidie kupata huduma anayoihitaji.
Kwa ujumla Jalsa iliandaliwa vizuri zaidi mwaka huu na kazi ya Afisa Jalsa salana ilikuwa nzuri sana. Jicho liwekwe kwa kila mapungufu yaliyojitokeza mwaka huu ili yaweze kurekebishwa mwakani. Mapungufu ya mwaka jana kama vile sauti yamerekebishwa mwaka huu. Khalifa Mtukufu aliwashukuru wahudumu wote.
Baadhi ya misikiti pia ilizinduliwa wakati wa safari ya Huzur nchini Ujerumani. Kwenye moja ya uzinduzi huo mkazi mmoja alisema ameshawahi kusikia moja ya hotuba ya Hazrat Khalifatul Masih aliyoitoa kwenye Bunge la Ulaya na sasa alikuwa na hamu kumsikiliza nini atasema katika ngazi ya kitongoji kwenye ufunguzi wa msikiti huo na akataka kuona je, Huzur anaongelea masuala ya amani akiwa kwenye ngazi za kimataifa tu na akiongea na watu mashuhuri? Lakini anasema, aligundua kimsingi yale yale aliyoyasema kwenye bunge la Ulaya ndiyo aliyoyasema wakati wa ufunguzi wa msikiti huu na jambo hili lilimvutia sana mkazi huyu. Kwenye ufunguzi huu Meya wa eneo hili pamoja na wageni wengine walitoa maoni yao.
Kwenye ufunguzi mwingine wa msikiti, Mkuu wa Mkoa alisema kuwa amevutiwa sana na hotuba ya Hazrat Khalifatul Masih. Alishauri kwamba hotuba hiyo iwekwe kwenye mtandao. Mama mmoja ambaye ni mbunge alisema kwamba amefurahi sana kupata nafasi ya kushiriki ufunguzi huo. Alisema: Juu ya uelewa mbaya ulioenea kuhusu Islam, ilikuwa ni muhimu kila mtu awepo kwenye ufunguzi huo na kutoa ujumbe wa amani. Mgeni mwingine alisema hapo kabla ilikuwa ni vigumu kwake kuwa na mtazamo chanya juu ya Islam, lakini baada ya kusikiliza hotuba ya Hazrat Khalifatul Masih sasa anaihesabu Islam kuwa ni dini ya amani. Mhandisi mmoja ambaye alishiriki kwenye ujenzi wa msikiti alisema anakubaliana na kila kitu Huzur alichokisema. Alisema kwenye tukio lote hajaona usanii wowote kama auonao kwenye hafla za kanisa.

Matukio yote haya yalitangazwa vya kutosha kwenye mtandao na vyombo vingine vya habari. Kwa ujumla watu milioni 106 hadi 107 wanakisiwa kufikiwa kupitia njia ya mtandao. Magazeti yaliyotoa habari hizi yanao wasomaji wanaofikia milioni 32. Aidha vituo vitatu vya Radio na vinne vya TV vilitangaza habari hizi. Kwenye siku ya mwisho ya Jalsa, mwanadada mmoja, mwandishi wa habari alifanya mahojiano na Huzur na habari zake zitachapishwa katika sehemu mbili kwenye mtandao.
Habari za ufunguzi wa msikiti wa mwisho zilitokea kwenye magazeti matatu ambayo yanao wasomaji kama 116,000.
Uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya msikiti mpya pia ulifanyika na habari zake zilichapishwa kwenye gazeti lililo na wasomaji wapatao milioni 6.
Mahojiano na Hazrat Khalifatul Masih pia yalifanywa na mtangazaji mmoja Mwanajumuiya. Mahojiano hayo yamewekwa kwenye mtandao ulio na wasomaji wapatao 1.5 milioni.
Wakati Jalsa salana inatusaidia sana kwa ajili ya maendeleo yetu ya kiroho wakati huo huo inatoa nafasi kwa wengine kupata ujumbe sahihi wa Islam. Watu wengi ambao hawakuwa tayari kufanya baiat hapo kabla walijisikia haja ya kufanya baiat baada ya kukutana na Hazrat Khalifatul Masih na kuuliza maswali. Hivyo kuna mambo mengi ya kutoa shukurani! Mwenyezi Mungu Aisaide Jamaat juu ya kuwaangalia ndugu hawa wapya na pia Ajaalie baraka za Jalsa zienee kwa mapana na marefu zaidi. Mwenyezi Mungu Amjaalie kila mshiriki wa Jalsa kupata manufaa yake ya kudumu. Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Ram./Shawwal 1436 AH | Julai 2015 | Wafa 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Jabir bin Abdillah r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Msijifunze elimu kwa nia ya kuona fahari mbele ya wataalamu wengine wala kwa kuringa mbele ya wasio na ujuzi na kuwagombanisha, wala msifanye vikao kwa kuonesha elimu yenu. Atakayefanya hayo atapata moto! Naam moto! (*Ubn Majah*).

Jalsa Salana Ujerumani 2015 yafungua milango zaidi ya baraka

Misikiti mitatu yazinduliwa

Na Mwandishi wetu

Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. amesema: Mtu awe mwenye kuomba muda wote na katika hali zote na pia ashike njia hii: **Na ama neema za Mola wako, basi uzisimulie kwa wingi** (93:12). Hili linaongeza mapenzi kwa Mwenyezi Mungu na kukuza subira, utii na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu.

Hazrat Khalifatul Masih (Kiongozi wa waaminio duniani) akasema: Katika kila safari yake nje ya nchi (Uingereza) Mwenyezi Mungu hufuangua milango zaidi ya neema Zake. Kwa fadhili Zake, Mwenyezi Mungu huibariki mipango yote na ujumbe wa kweli wa Islam unawafikia watu wengi zaidi nao hupata kuathirika. Lengo hasa la safari ya Huzur ya Ujerumani hivi karibuni ilikuwa ni kushiriki Jalsa salana ya Ujerumani, ingawaje mipango mingi pia ilipangwa ambapo kupitia hiyo Islam ya kweli ilihubiriwa kwa watu. Wakati neema za Mwenyezi Mungu zinakuja kuliko juhudi ya mtu na maombi yake hapo inakuwa ni wajibu zaidi kuzisimulia. Kwa namna ambavyo Jalsa salana na mipango mingine ilivyobarikiwa na Mwenyezi Mungu kuweza kufikisha ujumbe wa Islam Ahmadiyyat kwa watu wengi zaidi, inatukumbusha zaidi kusimulia baraka hizi. Jumuiya ya Ujerumani hususan inatakiwa itoe shukurani kubwa kwa Mwenyezi Mungu kwa jambo hili na wamgeukie Yeye zaidi ya hapo kabla. Haiwezekani kuzifikia nyoyo na akili za watu bila msaada wa Mwenyezi Mungu. Wakati mwingine hata hotuba nzuri nzuri haziwezi kuleta athari wakati maneno machache ya kawaida yakaleta athari kubwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu.

Masjid Baitul Qadir (ulioko katika mji wa Vechta), moja ya misikiti iliyozinduliwa hivi karibuni, wakati wa ziara ya Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. nchini Ujerumani.

Wageni waliofika kwenye Jalsa na hata wale waliofika kwenye mipango mengine (kama vile ufunguzi wa misikiti) walivutiwa sana na taratibu zilivyokuwa na mazingira kwa ujumla. Wageni wengi wanajumuiya waliohudhuria Jalsa ni wa kutokea Ulaya ya Mashariki na Magharibi kama ilivyo kwa wale wasio Waahmadiyya pia. Wageni walifika kutoka nchi kadhaa ikiwemo Macedonia, Croatia, Slovenia, Latvia, Belgium, Italy, Spain n.k. Waahmadiyya wenye asili mbalimbali waishio Ujerumani pia walifika kukutana na Huzur.

Wageni 16 walikuja kutoka Albania na wawili kati yao wakafanya Baiat. Mwanajumuiya mmoja alikuja na mke wake wote wawili ni wanasheria. Mke wake hakuwa amefanya Baiat kabla ingawaje alishamhubiria. Mama huyo alifanya Baiat kwenye Jalsa na akasema amejionea ladha ya kuhudhuria Jalsa kuwa ni jambo lisilo la kawaida. Alisema anatambua baadhi ya mazuri ya Islam kupitia Tabligh aliyofanyiwa na mume wake lakini amepata nguvu zaidi ya kujiunga baada ya kuhudhuria Jalsa na kukutana na Huzur. Aliendelea kububujikwa machozi kipindi chote pamoja na kwamba umri wake ni mdogo.

Mgeni mmoja pia kutoka Albania alitangaza wakati wa kukutana na Huzur kwamba anaikubali Ahmadiyya kwa moyo wote.

Mgeni mmoja kutoka Kosovo akasema kwamba mwaka jana pia alihudhuria Jalsa lakini ameona maandalizi ya mwaka huu kuwa bora zaidi.

Wageni 62 walifika kutoka Macedonia; 14 kati yao walikuwa ni Wakristo na 37 walikuwa waislamu wasio Waahmadiyya. Walisafiri kwa muda wa masaa 36 kufika kwenye Jalsa. Kwenye

Endelea uk. 11

Alama za kumtambua Imam Mahdi

Na Dawati la Kiswahili Morogoro

Mtume Muhammad saw alisema kwamba mnamo siku zetu hizi za mwisho watu watakapokuwa wameachana na imani na kukithiri kwa maovu, Mwenyezi Mungu Atamtuma duniani nabii atakayetokana na Waislamu, ambaye utume na majukumu yake yatafanana sana kiroho na yale ya nabii Isa a.s. kiasi ya kufahamika kama Isa wa mfano.

Nabii huyo pia atajulikana kwa lakabu ya Imam Mahdi, yaani Imam anayechaguliwa na kuongozwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu. Imam Mahdi ni cheo wapewacho manabii na mitume wa Mwenyezi Mungu (Kurani Tukufu Sura Anbiyaa 21:74). Mtume s.a.w. alisema kwamba huyo huyo Imam Mahdi ndiye atakayekuwa Isa bin Mariam, si watu wawili tofauti, pale aliposema:

Wa lal Mahdiyyu illaa 'Isa bni Maryama

Mahdi ndiye Isa bin Mariam (Ibnu Maaja, Kitaabul Fitan, Bab Shiddatiz Zamaani).

Sheikh Bakri Abedi Kaluta - Mkuu wa Dawati la Kiswahili, Morogoro Tanzania.

Huyo Imam Mahdi hatakuwa Muarabu bali Muajemi. Ndani ya Sura ya Al Jumua, imetolewa bishara kwamba, Mtume Muhammad s.a.w. atatumwa tena duniani kwa watu wengine walio bado kuungana nao, na alipoulizwa kwamba hao ni watu gani atakaotumwa kwao, aliuweka mkono wake juu ya bega la sahaba fulani ambaye hakuwa muarabu aliyeitwa Salman Farsi r.a., na kusema: kwamba imani itakapotoweka duniani mtu atakayetokana na watu wa Salman muajemi ndiye atakayeileta tena duniani. Akimaanisha kwamba kuna mtu wa shani ya juu sana atakayetumwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu kuja kuwarejesha watu kwenye imani ya kweli iliyoletwa na Mtume Muhammad s.a.w., na ujio wa mtu huyo, asiyekuwa mwarabu, utakuwa kama ndio ujio wa Mtume s.a.w. mwenyewe pale aliposema:

Lau kaanal iimanu mu'allaqan bith thuraiyya, lanaa lahuu rajulun au rijaalun min ahli Faaris yaani imani itakapotoweka duniani, basi ni mtu au watu watakaotokana na Waajemi ndio watakaotuletea tena imani. (Bukhari Kitaabut Tafsir chini ya aya Wa aakhariina minhum... (62:4), pale alipoulizwa kuhusiana na utabiri wa Kurani Tukufu kwamba yeye Mtume s.a.w. ametumwa pia kwa watu wengine wa baadae walio bado kuungana naye.

Mtume s.a.w. alisema kwamba jina la Imam Mahdi litakuwa ni Ahmad na atatokea India pale aliposema, kama ilivyosimuliwa na Hadhrat Anas bin Malik r.a. kwamba:

'Samiitu Khaliilii; laa taquumus saa atu hattaa yab 'athal Laahu ta'aala 'iswaabatun taghzul Hinda wa hiya takuunu ma'al Mahdiyyi ismuhuu Ahmad wa (hiya) 'iswaabatun takuunu ma'a Isa bni Maryama; yaani nilimsikia Rafiki yangu (akisema) kutakuwa na jeshi litakalopigana vita huko India, nalo litakuwa pamoja na Mahdi ambaye jina

Endelea uk. 10